SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**PROF.** Makubi asema serikali ina nia njema chanjo ya UVIKO-19




UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Desemba 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580802

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Hatua sita kukabili vifo vya mahabusu ya polisi

UKURASA 2



Baadhi ya abiria wanaoelekea mikoa mbalimbali nchini wakisubiri usafiri katika stendi ya Magufuli iliyoko Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam jana. Hata hivyo wengi wao wakiwa hawajavaa barakoa na hata kukaa kwa kuacha nafasi ili kujikinga na Uviko. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA WA 3

## WANAFUNZI 34 SHULE MBILI WAGUNDULIKA TATIZO MOYO

WANAFUNZI 34 kati ya 1,000 wanaosoma Shule za Msingi Mji Mpya na Muhimbili mkoani Dar es Salaam, wamebainika kuwa na matatizo ya moyo ikiwamo hitilafu ya valvu kwenye moyo. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kuanzia...

UKURASA WA 3

## NDUGAI: AIBU KWA TAIFA UMEME KUKATIKA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema anakerwa na tabia ya kukatika umeme na maji mara kwa mara kunakoendelea hivi sasa...



UKURASA WA 5

## JAFO ATOA MTIHANI KWA MANISPAA ULINZI DAMPO

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameelekeza Manispaa...

UKURASA WA 5

## GEREJI BUBU, 'CAR WASH' HOLELA MARUFUKU DAR

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amepiga marufuku gereji bubu na sehemu za kuoshea magari holela...

## Mhitimu SUA auawa, kisha mwili kutupwa shambani

UKURASA 2

## Dk. Mwinyi atumbua na kuteua watendaji wapya

UKURASA 2



Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Viwango vya Mahesabu ya Umma ya Kenya (PSASB), Stephen Masha, akimkabidhi Tuzo ya Uwasilishaji Bora wa Taarifa za Fedha kwa mwaka 2019/2020 katika sekta ya benki kwa ukanda wa Afrika Mashariki, Meneja wa Idara ya Fedha ya Benki ya CRDB, Aldo Kamugisha (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MICHEZO YANGA RASMI YAMNASA NKANE, SURE BOY AITWA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

## Mhitimu wa SUA auawa, mwili wake watupwa shambani

**Na Mwandishi Wetu**

MHITIMU wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) mkoani Morogoro, Magreth Mashue, ameuawa na watu wasiojulikana kisha mwili wake kutupwa kwenye shamba la chuo hicho.

Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (RCO) Mkoa wa Morogoro, Ralph Meela, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo alipotafutwa na Nipashe jana na kubainisha kuwa kwamba mwanafunzi huyo alihitimu chuoni huko Novemba 26, mwaka huu, akitunukiwa Shahada ya Sayansi ya Mazingira.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, Meela alisema kuwa msichana huyo alipotea tangu Desemba 14, mwaka huu, hadi Desemba 18, mwili wake ulipookotwa na wanakijiji katika pori la chuo hicho.

"Uchunguzi wa awali hadi sasa tumebaini kwamba shingo yake ilivutwa, tunamshikilia kijana mmoja ambaye alikuwa ni mpenzi wake wakati wote wakiwa chuoni, lakini uchunguzi bado unaendelea," alisema Meela.

Akifafanua sababu za kumshikilia kijana huyo, Meela alisema baada ya kutoweka kwa msichana huyo, kijana huyo hakuwahi kutoa taarifa yoyote kituo cha polisi na kwamba Desemba 13 wawili hao walikuwa pamoja. Mkuu wa Upelelezi huyo alibainisha kuwa wawili hao walikuwa wanaishi pamoja tangu binti huyo alipohitimu masomo yake na hakurudi nyumbani kwao katika kipindi chote hicho.

"Wawili hao walikuwa wapenzi, walikuwa wanaishi chumba kimoja. Baada ya kuhitimu masomo yake, binti huyo hakurudi nyumbani na hata Desemba 13 alimuaga mpenzi wake kwamba anakwenda kutafuta kazi Mzimbu Road," Meela alidai.

Ofisa Mawasiliano wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Scolastika Nduga, alikaririwa na vyombo vya habari jana akikiri hospitali hiyo kuupokea mwili wa binti huyo.

Serikali ya Wanafunzi ya SUA (SUASO) kupitia kwa Naibu Waziri wa Habari wake, Brian Ndossy, pia ilitoa taarifa iliyosomeka: "Serikali ya wanafunzi kupitia Wizara ya Ulinzi na Usalama inapenda kuwataarifu kwamba mwili wa dada uliookotwa karibu na mashamba ya mikonge Mazimbu, umebainika kuwa ni wa Magreth Liberath Mashue aliyehitimu masomo ya Sayansi ya Mazingira."

Pia ilidaiwa katika taarifa hiyo kuwa vipimo vya mwili vimeonyesha alipigwa na kubakwa na kwamba taarifa ya mipango ya mazishi ilitarajiwa kutolewa baadaye.

Kaka wa marehemu, Denis Mashue, aliliomba Jeshi la Polisi kuwatafuta watu wote waliohusika na kifo cha ndugu yake ili wachukuliwe hatua za kisheria kwa kuwa kitendo hicho kimeiumiza familia yao.

Alisema kifo cha ndugu yao kimewashtua kwa kuwa mara ya mwisho waliwasiliana naye Desemba 13, mwaka huu, alipowaomba fedha kwa ajili ya matumizi na kuwaahidi kuendelea na jitihada zake za kutafuta kazi katika baadhi ya kampuni baada ya kuhitimu.

***Imeandikwa na Idda Mushi, Frank Kaundula (MOROGORO) na Gwamaka Alipipi (DAR)**

# Hatua 6 kukabili vifo mahabusu ya polisi

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi limebainisha hatua sita linazozichukua kukabiliana na vifo vya watuhumiwa kwenye mahabusu ya jeshi hilo nchini.

Msemaji wa jeshi hilo, David Misime, alibainisha hatua hizo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe, iliyotaka kujua utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya Agosti 25, mwaka huu, kukabiliana na vifo hivyo.

Misime alisema kuwa baada ya Rais kutoa maelekezo hayo kwa Jeshi la Polisi, wamechukua hatua hizo zinazojumuisha kuwekwa mpango kazi wa kutekeleza maagizo hayo ili kudhibiti matukio ya vifo vya watuhumiwa walio mikononi mwa polisi.

Alisema hatua ya pili ni kuhuishwa kwa mafunzo kwa askari walio kazini na vyuoni, kuhusu kutotumia nguvu zaidi katika utekelezaji wa kazi zao za kila siku.

Misime alisema kuwa viongozi kuanzia ngazi ya vituo hadi mkoa, wamesisitizwa kusimamia askari kwa karibu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

Aliitaja hatua nyingine iliyochukuliwa ni kuwapo ukaguzi wa kila mara kuhusu utendaji wa kazi wa jeshi.

"Kumewekwa utaratibu endelevu wa utoaji elimu kwa kina, inayohusu haki za binadamu katika ngazi zote," Misime alisema.

Alisema hatua nyingine iliyochukuliwa ni msisitizo umetolewa kuhusu mantiki ya utumiaji nguvu inapobidi, ikioanishwa na mwongozo wa sheria husika na mazingira yake.

***Soma undani wa suala hili ukurasa wa 4**



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Jumuishi Temeke, Ilvin Mugeta, akizungumza katika mkutano wa wadau mbalimbali kuhusu jedwali la mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Mirathi ya Kimila ya Mwaka 1963 pamoja na masuala ya haki za ardhi kwa wanawake, ulioandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika ( WILDAF ) jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dk. Mwinyi atumbua na ateua watendaji wapya

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi wa viongozi katika Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale na kumtumbua Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii, Dk. Mohamed Abdallah.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mawaziri, Zena Ahmed Said, iliyotolewa jana, Dk. Mwinyi amemteua Hafsa Hassan Mbamba kuwa Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar.

Kabla Mbamba kuteuliwa, nafasi hiyo ilikuwa inashikiliwa na Dk. Mohamed Abdallah ambaye ameitumikia kwa kipindi cha miezi mitatu na siku saba.

Dk. Mohamed aliteuliwa na Rais Dk. Mwinyi kushika nafasi hiyo ya Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar Septemba 14 mwaka huu na uteuzi wake ulitenguliwa jana.

Ikumbukwe kuwa hivi karibuni, Rais Dk. Mwinyi, akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari Ikulu Zanzibar, alisema utendaji mzuri wa kazi ndiyo utakaombakisha mtendaji aliyemteua kwenye nafasi yake katika taasisi na mashirika ya umma.

Wengine walioteuliwa jana ni Mariyam Muhammed Hamid, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale na Dk. Abdallah Mohamed Juma, aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Utalii.

Wengine aliowateua ni Mohamed Manssor aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Masoko Kamisheni ya Utalii, na Omar Suleiman Mohamed aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi na Uratibu wa Shughuli za Utalii, Kamisheni ya Utalii.

Mwingine ni Aviwa Issa Makame aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Rasilimali Watu, Mipango na Utawala Kamisheni ya Utalii.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, akiangalia taka zinazotupwa katika dampo la kisasa la Manispaa ya Mtwara Mikindani wakati wa ziara yake ya kukagua usimamizi wa taka ngumu katika dampo hilo. PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS

# Prof. Makubi: Serikali ina nia njema chanjo ya UVIKO-19

**Na Christina Mwakangale**

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, amesema serikali ina njema kuwalinda wananchi dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 kupitia chanjo.

Prof. Makubi alitoa kauli hiyo jana mkoani Arusha alipozungumza na wenyeviti wa serikali za mtaa, vitongoji, kidini na kamati ya ulinzi na usalama kuelekea uzinduzi wa awamu ya pili ya uhamasishaji chanjo ya UVIKO-19 unaotarajiwa kufanyika leo.

Alisema serikali ina nia njema ya kuwalinda wananchi ili waendelee na shughuli za uzalishaji mali, hivyo itaendelea kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo na kutoa chanjo.

Prof. Makubi alisema kampeni ya awamu ya pili ya mpango shirikishi na harakishi wa uhamasishji chanjo dhidi ya UVIKO-19, inayoanza leo, inalenga kuwafikia wananchi ili kupata kinga na kufikia asilimia 60 ya kinga kwa muda mfupi.

"Hakuna chanjo iliyofanikiwa kwa kulazimisha, bali kwa kuelimishana na wananchi na kuelewa sayansi, hivyo baadaye mtu kuamua kuchanja kwa hiari yake," alisema.

Prof. Makubi alibainisha kuwa kampeni hiyo itajumuisha viongozi wa mitaa watakaopewa majukumu hayo na ndio sababu serikali imeamua kushusha huduma ya chanjo kwa wananchi mtaani.

Alifafanua kwamba kampeni ya mtaa kwa mtaa haileti ulazima, bali kupeana elimu ngazi ya mtaa na wananchi, na kwa hiari yao kwenda kupata chanjo.

Prof. Makubi pia alisema kuwa mbali na chanjo, wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari kwa kunawa mikono mara kwa mara na maji tiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuvaa barakoa.

"Jambo lingine niwakumbushe wananchi kufanya mazoezi pamoja na kula lishe bora, kwani mazoezi ni muhimu na inasaidia mifumo ya hewa kuwa mizuri," alisema Prof. Makubi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, alisema wakati nchi ikielekea kwenye sikukuu za mwisho wa mwaka, ni muhimu kushirikishana na viongozi wa dini, mitaa na kimila, ili kuwa na namna bora ya kuwafikia wananchi kwa kuwalinda, hasa wazee walioko majumbani.

Prof. Shemdoe pia aliwataka viongozi hao kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa chanjo ya UVIKO-19 na kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo.

## Wanafunzi 34 shule mbili wagundulika tatizo moyo

**Na Christina Mwakangale**

WANAFUNZI 34 kati ya 1,000 wanaosoma Shule za Msingi Mji Mpya na Muhimbili mkoani Dar es Salaam, wamebainika kuwa na matatizo ya moyo ikiwamo hitilafu ya valvu kwenye moyo.

Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kuanzia Februari hadi Mei mwaka 2019, ulilenga kubaini iwapo kuna watoto wanaougua magonjwa ya Valvu za Moyo (RHD) bila ya kuwa na dalili zozote.

Utafiti huo umeongozwa na Bingwa wa Magonjwa ya Watoto kutoka JKCI, Dk. Parvina Kazahura.

Mratibu wa Utafiti kutoka JKCI, bingwa wa magonjwa ya moyo, Dk. Pedro Pallangyo, akizungumzia utafiti huo ambao umetolewa wiki hii, alisema utafiti huo ulilenga shule za msingi kwa wanafunzi 949 ambao hawana dalili ya magonjwa ya moyo na kufanyiwa kipimo cha echo (echocardiographic).

"Lengo la utafiti huu ilikuwa kubaini mapema watoto waliopata maambukizi mapema kwenye mfumo wa valvu za moyo na kupata matibabu mapema. Pia uliangalia visababishi gani na hatarishi kwa watoto walio na makovu kwenye valvu za moyo.

"Tuligundua sababu tatu, watoto waliokuwa na umri wa miaka tisa na kuendelea walikuwa katika hatari ya kuwa na matatizo haya ikilinganishwa na walio chini ya umri huu, pia waliopata maambukizi, katika mfumo wa hewa, kikohozi, mafua zaidi ya mara tatu miezi sita kabla ya utafiti huu, uwezekano ulikuwa mkubwa wa kuwa na tatizo la valvu," alisema bingwa huyo.

Alisema sababu nyingine kwa tatizo hilo ni uchafuzi wa hali ya hewa ambao unaongeza uwezekano wa magonjwa ya mfumo wa hewa na kusababisha uwezekano wa magonjwa ya valvu.

Bingwa huyo alitaja sababu nyingine ni hali duni za maisha, akibainisha kuwa asilimia 29.5 hadi 32.9 ya upasuaji wote wa moyo uliofanyika JKCI mwaka 2017 na 2018, ulitokana na wagonjwa kuwa na tatizo la valvu kwenye moyo.

# Ndugai: Aibu kwa taifa umeme kukatika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema anakerwa na tabia ya kukatika umeme na maji mara kwa mara kunakoendelea hivi sasa katika maeneo mengi nchini.

Alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akichangia mada katika kikao cha Kamati ya Ushauri Mkoa wa Dodoma (RCC).

Alisema tabia ya kukatika kwa umeme katika maeneo mbalimbali inatia aibu taifa kwa kuwa mataifa mengi duniani yameshavuka katika hali hiyo.

"Unakuta eti unawasha taa hakuna umeme au unafungua koki ya bomba la maji hakuna maji, hali hii haipo duniani suala kama hili la huduma wenzetu walishavuka siku nyingi mtu akifungua koki anatakiwa akute maji na siyo vinginevyo.

"Lakini hatuwezi kuwalaumu kwa sababu hatujui nini tatizo, lakini katika suala la umeme kama kule kwangu Kongwa aisee imekuwa kero kubwa sana, mara unawaka mara unakatika na tena wakisikia Simba kamfunga Yanga ndiyo haurudi kabisa," alisema kwa utani.

Kadhalika, Ndugai aliwataka wajumbe wa kikao hicho kuweka mikakati ya kwenda kukabiliana na kero ya mimba za utotoni.

Alisema kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa katika kikao hicho, mimba za utotoni zimeongezeka kila mwaka hali ambayo inahitaji juhudi kuchukuliwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Emmanuel, alisema Shirika la Umeme nchini linatakiwa kubadilika kwa kuwa hali hiyo inachonganisha wananchi na serikali yao.

Alisema Wilaya ya Kongwa hivi sasa upo uwekezaji wa viwanda, lakini kutokana na hali ya kukatika kwa umeme inaathiri shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

"Kitendo hicho kinachofanywa na wenzetu TANESCO kukata umeme mara kwa mara, wakati mwingine unakatika hata mara tano kwa siku, hali hii inawachonganisha wananchi na serikali yao, lakini pia bidhaa za watu nyingi zinaungua," alisema Emmanuel.

Juzi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme, Maharage Chande, alisema hakuna mgao wa umeme na kama kuna mahali umeme haupo kuna matengenezo au 'Transformer' limeharibika.

Alisema kwa sasa mvua inanyesha vyanzo vingi vya maji vimejaa na kuruhusu uzalishaji kuendelea kama kawaida, na kwamba mwezi Novemba hali ilikuwa mbaya zaidi kutokana na ukame.

Katika kikao hicho Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, alisema pamoja na changamoto ya mimba za utotoni nyingine ni watoto wa kike kuacha masomo na kufifisha ndoto zao za maisha.

"Lazima tuwe na mikakati ya kuwatafuta watoto hawa ambao wamekuwa wakiacha masomo, hawa ndiyo sababu ya hizi mimba za utotoni mkoani hapa," alisema Dk. Mganga.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMISTRATION CAUSE
NO……………………………………2021
In the Matter of the Estate of the late LISA MICHAEL MWANGUPILI of area "A" within
Dodoma Region
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BISE NELSON MWAIPOPO
GENERAL CITATION
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 Day of January 2021

Date at Dodoma this 2 Day of December 2021
Presented for filing this 14 day of 12/ 2021

COURT SEAL

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA REGION

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL
The Registration of Documents Act.
(CAP.117)**

BY THIS DEED, I the undersigned ZAITUNI WENDY MUSETTI of P.O.BOX 5287, MWANZA DO HEREBY absolutely renounce and abandon the use of my former name of ZAITUNI WENDY MUSETTI NG'ARIBA which appears on my marriage certificate, TIN 113-997-745, National Identification Card number 197880804-33102-00001-16 and also on my NMB Bank Account number 31110008764 and CRDB Bank Account number 01J2418100400, CRDB Bank Account number 152018100400. In lieu thereof do assume and adopt the name of ZAITUNI WENDY MUSETTI which appears on my secondary living certificates and birth certificate.

And IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall at all times hereinafter in all records, deeds and instruments and upon all occasions whatsoever, use and sign the said name of ZAITUNI WENDY MUSETTI as my name in lieu of the said name ZAITUNI WENDY MUSETTI NG'ARIBA

And I HEREBY AUTHORIZE and request all persons to designate and address me by such assumed name of ZAITUNI WENDY MUSETTI only.

SIGNED and DELIVERED by the said ZAITUNI WENDY MUSETTI who is known to me personally/identified to……………………… me by……. the later being known to me personally in my presence this………... day of……………………………2019 — **DEPONENT**

NAME:
SIGNATURE:
ADDRESS P.O. BOX 331 MWANZA
QUALIFICATION: STATE ATTORNEY

RIPOTI MAALUMU - 3

# Kitendawili cha usalama mahabusi walioko polisi

## • Agizo la Rais Samia, sheria ilikosimama
## • Polisi watii, waja na hatua 6 kutekeleza

**Na Waandishi Wetu**

***SEHEMU ya pili ya ripoti hii jana iliangazia kwa kina ushuhuda wa kinachojiri mahabusu, hadi miili inayowasilishwa hospitalini na vitendawili vyake, baadhi vigumu kuvitafsiri. Nini mwelekeo mpya? Endelea na sehemu ya mwisho ya ripoti hii:***



Rais Samia Suluhu Hassan



IGP Simon Sirro

**ALICHOKIBAINI RAIS**

Mnamo Agosti 25, mwaka huu, Rais Samia kwenye Bwalo la Maofisa wa Polisi Oysterbay mkoani Dar es Salaam alipokutana nao, aliwaonya kwa marejeo ya kina kuhusu madhila, hata vifo vya watuhumiwa mikononi mwa polisi.

Alitamka: "Baadhi yenu mnashtumiwa kwa kutotenda haki. Ninaomba mwangalie vitendo vinavyofanywa. Na inapotokea hivi, tunasimama haraka kujitetea kama jeshi bila kuangalia haki za jamii.

"Kuna mifano kadhaa. Ninadhani miezi miwili mitatu nyuma kulikuwa na unyang'anyi wa nyama eneo moja Dar es Salaam hapa. Mlivamia bucha, mkachukua nyama za watu, walipolalamika mkasema 'aah tumefanya vile kwa sheria', lakini ukiangalia kwa undani kilichotendeka, hakuna sheria hapo.

"Kwa hiyo, lazima mwangilie hilo na mengine na mengine! Tupo hapa kuhudumia watu, siyo kudidimiza watu!

"Lakini lingine, mtuhumiwa anapokufa mikononi kwako askari wa polisi, umemchukua huko, umemburuza, umeshamchapa virungu vya kutosha na nini.

"Wanadamu sisi tuko wa afya tofauti tofauti. Kuna mwingine chapa, chapa na chapa, yupo ngangari. Mwingine vifimbo viwili tu tayari hayupo, ameshafika mbele ya haki.

"Kwa hiyo, ninadhani matumizi ya nguvu, IGP na yenyewe muyatazame. Kesi za watu kufa vituo vya polisi hazileti sifa nzuri kwa serikali. Ninaomba sana ndugu zangu tendeni yaliyo haki."

Katika hadhira tofauti miezi minne baadaye, tarehe 12 mwezi huu, Mkuu wa Nchi alirejea tena angalizo lililoendana na maelekezo ya haja ya nidhamu na utii wa sheria katika utendaji wa polisi, akitoa mfano wake binafsi kuwa miongoni mwa watendwa wa madhila hayo.

**WANASHERIA LHRC**

Ripoti ya mwaka jana ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ilibainisha mwaka huo ulikuwa na matukio sita ya utesaji na kutendwa isivyo kati ya raia na vyombo vya dola.

Ni matukio yaliripotiwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam na Mara.

LHRC katika ripoti ya utafiti wake unaohusu haki za binadamu, ilitaja asilimia 8.8 ya washiriki walisema uwezekano wa kufanyiwa utesaji/kutendwa vibaya wakiwa chini ya ulinzi ni mkubwa kiasi, huku asilimia 33.5 wakisema ni mkubwa.

Mkurugenzi wa LHRC, Anna Henga, anasema utafiti huo umebaini ni matukio endelevu kila mwaka.

Anafafanua maudhui ya ripoti kwamba yanataja kikwazo cha kutokoma mwenendo huo, ni serikali kushindwa kuridhia Mkataba wa Kimataifa dhidi ya mateso kwa raia.

Pia analalamikia katiba iliyopo haijatoa fursa ya kuwapo mamlaka maalumu ya kulichunguza Jeshi la Polisi, hali inalolipa uhuru wa kujichunguza lenyewe dhidi ya tuhuma zake.

> **"Hakuna kitu muhimu kwetu kama kusimamia sheria na kutenda haki." IGP Simon Sirro, Novemba 21, 2021**

"Yanahitajika mabadiliko ya katiba ambapo hili ni jambo la muda mrefu. Jambo la muda mfupi, ni Tume ya Utawala Bora ifanye hiyo kazi.

"Pia iunde jopo maalumu ambalo halihusiani na polisi, wajumbe wa jopo hili hawatakuwa na mgongano wa kimaslahi, kwa sababu mengi yanachunguzwa lakini husikii hatua zilizochukuliwa," anasema Anna.

**WATETEZI WA HAKI**

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, anataja mbinu za kukabiliana na unyanyasaji kutoka kwa askari, zikijumuisha serikali kuridhia mikataba ya kimataifa inayopinga ukatili kwa wananchi.

Anaungana na mtangulizi wake (Anna), akitaka kuwapo mfumo au chombo huru ambacho kitaruhusu kamati huru kukagua matukio au malalamiko yanayofanywa na polisi. Mtazamo wake ni kuwa na mfumo ambao utakuwa na msaada wa udhibiti na hatua kuchukuliwa dhidi ya wasimamizi wa kisheria waliomo kwenye vyombo vya dola.

**MSIMAMO WA IGP**

Kama ilivyo nadharia ya kiaskari duniani inayotamka 'quest of command is the commanding question', ikimaanisha ombi kutoka kwa mwenye mamlaka linabeba sura ya maelekezo, Novemba 21 mwaka huu, IGP Sirro alitoa maelekezo kwa wasaidizi wake.

Ikiwa ni wastani wa miezi mitatu tangu kutolewa kwa karipio la Rais Samia dhidi ya vifo vya watu kwenye vituo vya polisi, IGP Sirro, akisimamia nadharia ya 'utii na nidhamu', aliwaagiza wasaidizi wa mamlaka yake kutenda haki kwa watuhumiwa wawapo mikononi mwa polisi.

Akiwa kwenye Chuo cha Polisi Moshi mkoani Kilimanjaro siku hiyo, IGP Sirro alielekeza watuhumiwa waheshimiwe na watendwe haki katika haiba ya watu wasio na hatia, mpaka itakapobainika vinginevyo.

"Hakuna kitu muhimu kwetu kama kusimamia sheria na kutenda haki, kuwa wanyenyekevu na kuheshimu watu. Sisi leo tumevaa majoho haya na kesho tunarudisha kwa wenyewe na wenyewe ni Watanzania wanaolipa kodi inayotufanya tufanye kazi," alihitimisha.

**HATUA 6 ZA POLISI**

Msemaji wa Polisi, David Misime, aliiambia Nipashe mwishoni mwa wiki iliyopita namna agizo la Rais lilivyopokewa na hatua sita zilizokwishaanza kuchukuliwa kurekebisha kasoro.

Kwa mujibu wa Misime, hatua hizo zinajumuisha kuandaliwa mpango kazi wa jeshi unaohusu njia sahihi za kutekeleza majukumu yao pasipo ama kukwaza au kuionea jamii.

Pia yanaambatana na kuandaliwa mafunzo maalumu vyuoni na kazini kuhusu kuepuka utumiaji wa nguvu kazini kadri inavyowezekana; mamlaka za mikoa na wasaidizi wake kuwa na ufuatiliaji wa karibu sehemu za kazi.

Vilevile, inaelekezwa kuwa uongozi wa kipolisi ufanye ukaguzi wa kila mara vituoni kubaini kila kinachoendelea sehemu za kazi; jeshi kutoa elimu endelevu ya haki za binadamu; na kukisisitizwa utii wa sheria na kuwapo mantiki za kisaikolojia na kisheria katika matumizi ya nguvu.

**HATUA SITA ZA POLISI**

1. Jeshi la Polisi liliweka mpango kazi wa kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Rais siku hiyo likiwapo la matukio ya watu kufia mikononi mwa polisi.
2. Mafunzo kazini na vyuoni kwa askari yamehuishwa zaidi juu ya matumizi ya nguvu katika utekelezaji wa kazi za polisi za kila siku.
3. Viongozi kuanzia ngazi ya vituo hadi mkoa wamesisitizwa kusimamia askari kwa karibu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.
4. Kufanya ukaguzi wa kila mara katika utendaji wa kazi.
5. Tumejiwekea pia utaratibu wa kuendeleza utoaji wa elimu juu ya haki za binadamu kwa nguvu zaidi katika ngazi zote.
6. Msisitizo umetolewa kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, pale inapobainika nguvu zaidi kutumika bila kuzingatia uwiano wa nguvu kutoka upande mwingine.

**Chanzo**: Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime

HABARI KITAIFA

## Gereji bubu, 'car wash' holela zapigwa marufuku Dar

Na Maulid Mmbaga

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amepiga marufuku gereji bubu na sehemu za kuoshea magari holela pembezoni mwa barabara.

Akizungumza jana na watendaji wa kata na wenyeviti wa mitaa jijini humo, aliwataka viongozi hao kuchukua hatua kwa wote wanaofanya shughuli hizo huku akisisitiza usafi endelevu kwa manufaa ya wote.

Aidha, aliwapa fomu maalum ya kufuatilia mwenendo wa utekelezaji wa agizo hilo ili kuongeza chachu ya uwajibikaji kwa viongozi.

"Pia nipige marufuku uendeshaji wa shughuli za biashara kwenye bustani, niwatahadharishe wale wote wenye tabia ya kuiba vyuma vilivyowekwa pembezoni mwa barabara, atakayebainika kuiba atachukuliwa hatua," alisema.

Kwa mujibu wa Makalla, watendaji wanatakiwa kuhakikisha mitaa yao ni misafi muda wote, takataka zinaondolewa kwa wakati, kudhibiti biashara holela na kuzuia wafanyabiashara wadogo wasirudi kusikoruhusiwa.

Pia Makalla alitoa maelekezo kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwa na mpango wa kushiriki kampeni ya usafi.

"Serikali inakwenda kufanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kupitia utafiti wa sekta isiyo rasmi wa mwaka 2019 ili kupata tija kwa kundi hilo, pia utafiti huo umewezesha mkoa kujua changamoto na fursa za kufanyiwa kazi ili kuongeza makusanyo ikizingatiwa kuwa mkoa wetu unachangia asilimia 18 ya pato la taifa," alibainisha.

Kwa upande wake Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoka (NBS), Dk. Albina Chuwa, alisema utafiti huo umebaini kuwa thamani ya shughuli zisizo rasmi ni zaidi ya Sh. bilioni 6, huku akibainisha kuwa wanawake wengi ndio wameonekana kujihusisha nazo ambapo Wilaya ya Ilala na Temeke ndiyo zinaongoza kuwa na shughuli hizo.

# Watiwa mbaroni kwa madai kumpiga polisi

Na Jaliwason Jasson, MANYARA

VIGOGO wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika Wilaya ya Babati Vijijini mkoani Manyara, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumshambulia askari polisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, aliwataja vigogo hao kuwa ni Katibu wa Wilaya, Filbert Mdaki (52) na Katibu wa Umoja wa Vijana (UVCCM) Wilaya, George Sanka (46).

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kuzaga alisema viongozi hao walimshambulia Koplo Baraka wa kituo kidogo cha polisi Kiru akiwa kwenye majukumu yake ya polisi kata.

Alisema tukio hilo lilitokea Desemba 12 katika kijiji cha Kirudiki ambako askari huyo alishambuliwa kwa kupigwa mateke na fimbo na Mdaki na Sanka kwa kushirikiana na wananchi mbalimbali wanaodaiwa kuwa wafuasi wa CCM.

"Ni kwamba watuhumiwa hao walikwenda kufanya mkutano wa hadhara pasipo kuwapo na taarifa yoyote katika kituo cha polisi wala hawakuwa na kibali," alisema Kuzaga. Alisema askari huyo alikwenda kwa ajili ya kutambua mkusanyiko huo na ndipo wanasiasa hao na wafuasi wao walipoanza kumfukuza kutaka aondoke eneo hilo na kuanza kumshambulia.

Kamanda Kuzaga alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.

Mmoja wa maofisa wa CCM ambaye hakutaka majina yake kutajwa alisema si kweli bali makatibu hao walikuwa wakimtetea askari dhidi ya raia waliokuwa wakimshambulia.



Jamii ya wafugaji wa Kimasai, Kitongoji cha Mlembule, Kijiji cha Mvungwe wilayani Kilindi mkoani Tanga wakifunga kamba ya ngozi ya kondoo mweusi kwenye Mto wa Kwambalazi kama tambiko la kumwomba Mungu ili mvua inyeshe. PICHA: DEGE MASOLI

# Jafo atoa mtihani kwa manispaa ulinzi dampo

Na Mwandishi Wetu, MTWARA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, ameelekeza Manispaa ya Mtwara Mikindani kuhakikisha inalinda eneo la dampo la kisasa lililojengwa, ili lisivamiwe na wananchi.

Dk. Jafo alitoa maelekezo hayo juzi alipozuru kikazi katika dampo hilo mkoani Mtwara lenye eneo la ukubwa wa ekari 23, waziri huyo akikagua namna wanavyosimamia taka ngumu.

Alisema baadhi ya wananchi wana tabia kuvamia maeneo yaliyo karibu na madampo kisha kujenga nyumba na kufanya makazi na huishia kutupa lawama kwa serikali ya eneo husika kuhusu harufu mbaya inayotokana na taka hizo.

Alisema serikali ilitafuta fedha ili kuhakikisha madampo yanajengwa katika maeneo mengi nchini katika kuhakikisha kunakuwapo na usimamizi mzuri wa taka ngumu.

Waziri Jafo alitumia nafasi hiyo kuipongeza manispaa hiyo kwa kuwa na usimamizi mzuri wa taka zinazotupwa katika dampo hilo, hali inayosaidia kutunza mazingira ya mji.

"Nimekuja kuangalia dampo hili namna mnavyozishughulikia taka ngumu na kweli nimekuta taka zote zinatupwa hapa tofauti na baadhi ya madampo huko nilikopita ambako taka hazitupwi kabisa kwenye dampo, zinaachwa zinazagaa ovyo," alipongeza.

Ofisa Mazingira wa Manispaa hiyo, Masumbuko Mtasigwa, alisema yapo malori manne ambayo yanatumika kusafirisha taka kutoka katika vizimba 25 vilivyoko katika kata 18.

Hata hivyo, alibainisha kikwazo cha gharama za uendeshaji kwa maana ya usafirishaji kupitia malori hayo pamoja na uwapo wa taka nyingi za plastiki zinazotupwa.

Meneja wa Kanda ya Kusini wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Boniface Guni, alisema kero ya matumizi ya mifuko midogo ya plastiki isiyo na viwango bado ipo.

Alisema hiyo ni kutokana na kuingia kwa magendo lakini baraza hilo linaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya mifuko mbadala iliyo rafiki wa mazingira na kuendesha operesheni ya kukamata mifuko iliyopigwa marufuku.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Polisi wahamasishe kujikinga UVIKO-19 kwenye mabasi

**HIVI** karibuni serikali imewataka Watanzania watakaosafiri kwenda likizo maeneo mbalimbali nchini, kuchukua tahadhari ya UVIKO-19 kwa kuvaa barakoa, kukaa umbali wa mita 2 kati ya mtu mmoja na mwingine na kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara.

Pia, kuwalinda wazee na watu wengine wenye maradhi yasiyoambukiza ambao ni kundi lilolo hatarini zaidi kwa kipindi hiki ambacho kuna mikusanyiko ya watu.

Kadhalika, wazazi wametakiwa kuwalinda watoto walio kwenye kipindi hiki cha likizo ambao watasafiri kwenda maeneo mengine nchini, kwa kuhakikisha wanavaa barakoa, kunawa mikono na kuepuka misongamano.

Tangu kugundulika kwa ugonjwa wa UVIKO-19 matangazo ya kuwataka wananchi kuchukua tahadhari ni mengi, na yamezidi zaidi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kuwa Tanzania kuna ugonjwa huo, akaonyesha mfano kwa kuchanja na kuvaa barakoa kila anapokuwa kwenye mikusanyiko.

Kwenye vituo vya mabasi kuna vyombo vya kunawa mikono ambavyo havitumiki, licha ya hamasa ya kuchukua tahadhari watu hawavai barakoa wala kutakasa mikono wanapokuwa kwenye mikusanyiko.

Tunashauri serikali kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa agizo lake ili kuepusha janga kwa wazee na makundi mengine yaliyo kwenye hatari huko vijijini, kwa kuwa wengi bila kujua hawatakumbuka kunawa au kuvaa barakoa.

Utekelezaji ni pamoja na kukagua mabasi mara kwa mara kama watu wanavaa barakoa na ikiwezekana kuchukua hatua kwa makondakta na madereva ambao hawahimizi uvaaji barakoa.

Mabasi mengi kwa sasa yana viyoyozi (AC) na watu wanakaa kwa zaidi ya saa tatu safarini, ni kawaida kukuta basi zima hawajavaa barakoa na wanashuka vituo mbalimbali, jambo ambalo ni hatari kwa kuwa wataalamu wanatueleza kuwa kirusi hicho huimarika zaidi kwenye baridi.

Ili kufanikisha utekelezaji ni lazima kuwe na ufuatilia wa karibu wa mabasi kutoa matangazo ya mara kwa mara kwa abiria kuvaa barakoa, lakini Polisi wa Usalama Barabarani pamoja na mambo mengine wanayokagua ni vyema wakahimiza uvaaji barakoa au mabasi kufungua vioo ili hewa ya asili iingie.

Mathalani, Nipashe ilitembelea Kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli na vingine nchini na kubaini kuwapo kwa vyombo vya kunawa mikono, lakini havitumiki, msongamano mkubwa wa watu na wengi hawavai barakoa jambo linalosababisha maambukizi kusambaa.


Nguvu inayotumika kuhimiza watu kuvaa barakoa wanapokuwa ndani ya viwanja vya ndege, boti na wanapoingia kwenye ofisi za serikali, sasa ielekezwe kwenye vyombo vya usafiri wa barabara na masoko ili kuepusha kusambaa kwa kirusi hicho, hasa katika kipindi hiki tunachoelezwa kuwa kuna kirusi kipya cha Omicron.

Kwa kuvaa barakoa, kuchanja na kunawa mikono mara kwa mara kumesaidia baadhi ya nchi zilizo mstari wa mbele kwenye kukinga raia wake dhidi ya UVIKO-19 kama Uingereza kuruhusu mashabiki wa mpira kuingia uwanjani bila barakoa kwa kuwa wamefanikiwa kuchanja watu wote.

Hii ni uthibitisho kuwa ikiwa tahadhari itachukuliwa inavyotakiwa basi tutafanikiwa kupambana na UVIKO 19 hasa kipindi hiki watu wanaposafiri kwenda kwenye sikukuu za mwisho wa mwaka.

Hadi Desemba 18, mwaka huu, jumla ya wananchi 1,275,795 sawa na asilimia 2.21 walikuwa wamepata chanjo ya Uviko-19, huku lengo likiwa ni kufikia watu milioni 35 sawa na asilimia 60.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Zamu wanasiasa kuwahimiza wamachinga kuuzia sokoni

Na Sabato Kasika

**NI** zaidi ya mwezi sasa, tangu kuondolewa kwa wafanyabiashara wadogo katika maeneo yasiyo rasmi kwenye majiji na miji, lakini baadhi yao wameibuka na mbinu ya kuendelea kubaki katika maeneo ya awali hasa Dar es Salaam.

Badala ya kwenda kwenye masoko waliyotengewe, wanakuwa mafichoni, katika baraza za nyumba za watu kuanzia asubuhi hadi saa 11 jioni ambapo huibuka na kurejea katika maeneo ya awali.

Machinga hao ni wale ambao wana meza za biashara kwenye masoko mapya na wengine wanaodai kuwa bado hawajapata nafasi katika masoko hayo, ambao wote kwa pamoja wamekuwa wakitumia mbinu hiyo.

Kwa mtazamo wangu naona kuna haja hata wanasiasa kushiriki katika kazi ya kuhamasisha machinga kuhamia kwenye masoko ili waweze kuendesha shughuli zao bila kuhangaika huku na kule.

Ninawataja wanasiasa kwa sababu wanawashawishi wasihame, lakini kwa kuwa sasa serikali imeamua kuwapanga vizuri, ili wafanye shughuli zao bila usumbufu, basi wanasiasa hawana budi kushirikiana na serikali.

Ikumbukwe kuwa, baadhi yao wanakiri kuwa na meza za biashara katika masoko mpya, na huweka vitu vichache ili waonekane wapo na kisha wanaondoka na kwenda kufanyia biashara vichochoroni.

Wenye mtindo huo ni machinga wa Mbezi Mwisho ambao kuanzia muda wa asubuhi hadi saa 10 jioni, huwa wako mafichoni, lakini kuanzia saa 11 jioni huibuka kutoka huko na kurudi kwenye maeneo walioondolewa.

Kwa sababu machinga ni wapigakura, basi ingependeza kama wanasiasa wangeshirikiana na serikali kutaka wahamie kwenye masoko rasmi kuliko kupoteza muda mwingi wakivizia nyakati za jioni.

Machinga wamekuwa wakiondolewa kwenye maeneo ya awali kisha wanarudi mmoja baada ya mwingine huku wanasiasa wakitajwa kuhusika katika kuwa ushawishi wa kuwarudisha katika maeneo ya awali.

Ikumbukwe kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ameshatangaza kuwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi itakuwa siku maalumu ya kufanya usafi kwa wakazi wa mkoa huo, akisema hayo hivi karibuni katika uzinduzi wa mkakati wa usafi na uhifadhi mazingira wa mkoa huo uliopewa jina la 'Safisha Pendezesha Dar es Salaam'.

Machinga ni miongoni mwa watu ambao wanatuhumiwa katika uchafuzi wa mazingira, hivyo kwa hali kama hiyo ingependeza kama watashawishiwa ili waende kwenye masoko waliotengewa.

Wanasiasa ni muhimu katika ushawishi kama ambavyo huwa wanafanya wanapotafuta kura kwa machinga kwa kuwabembeleza licha ya kwamba yapo malalamiko mengi ya machinga kwamba masoko mapya hayana miundombinu muhimu kama maji, vyoo na pia ukosefu wa wateja ambao unasababisha waendelee kuwa katika maeneo ya awali, na kuongeza mtifuano.

Pamoja na hayo, ni muhimu wanasiasa wawaelimishe kujua kwamba haki inakwenda sambamba na wajibu, ili kwamba badala ya kudai haki tu, watimize wajibu wa kuhama huku mipango zaidi ikiendelea.

Wakitambua hilo, wataachana na mtindo wa kunyang'anyana kisu na mtu huku wao wakiwa wameshika makali na kukatwa vidole.

Aidha, machinga wanatajwa kama wafanyabiashara muhimu na ni suluhisho la mahitaji kwa watu wengi kuanzia wa kipato cha chini, kati na cha juu, na wana umuhimu katika kukuza pato la taifa.

Ninaamini kwamba, badala ya kuendelea kufukuzana na serikali, wakielimishwa na kuelewa, wanaweza kutulia sehemu moja na kukuza uchumi wao na hata wa taifa na kusaidia kuondoa umaskini.

## Bonyokwa yapata msaada vifaa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Sekondari Bonyokwa iliyoko Tabata mkoani Dar es Salaam, imekabidhiwa vifaa vya masomo ili kupunguza tatizo la mahitaji ya vifaa vya elimu.

Vifaa hivyo ni meza na viti vya walimu, kabati la vitabu na mafaili, kompyuta mbili na printa.

Kampuni ya simu za mkononi ya Halotel ilitoa msaada huo jana.

Akitoa taarifa hiyo wakati akikabidhi vifaa hivyo, Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mawasiliano wa Kampuni hiyo, Sakina Makabu, alisema wameamua kusaidia vifaa hivyo kutokana na changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Alisema mpango huo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuhakikisha shule zote nchini zinapata mahitaji na vifaa muhimu vitakavyowezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira bora ili kukuza kiwango cha ufaulu wa wanafunzi hao na kupunguza uhaba wa vifaa vya elimu kwa shule zote nchini.

"Halotel tumeamua kutoa msaada huu wa vifaa ikiwa ni mojawapo ya mwitikio wa kampuni yetu wa kuitikia juhudi za serikali katika uboreshaji wa mazingira na upatikanaji wa vifaa vya ufundishaji na kujifunzia ili kuongeza ufanisi wa kufundishia na kujifunzia katika mfumo wa nadharia na vitendo," alisema Sakina.

Sakina alisema, Kampuni ya Halotel inatoa huduma ya kimasomo ijulikanayo kama 'Halostudy' itakayo wawezesha wanafunzi nchini kusoma masomo yao kwa njia ya mtandao (TEHAMA) inayopatikana kwenye simu za mkononi na kwenye kompyuta.

Alisema huduma hiyo inatumiwa na wanafunzi na walimu kote nchini bure, na kupitia kompyuta zilizotolewa Shule ya Bonyokwa itaweza kutumia huduma hiyo kitakacho hitajika ni kuwa na intaneti.

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo, Upendo Mgaza, alisema wamefarijika kwa kupokea msaada huo kutoka kampuni hiyo na wanashukuru kwa kuendelea kuwa karibu na jamii na kuthamini pia kwa kuunga mkono jitihada za kuisaidia sekta ya elimu nchini.

"Nina amini kabisa vifaa hivi vitawasaidia walimu na wanafunzi hapa shuleni katika kuboresha namna ya ufundishaji na kujifunza kwa ujumla".

Kampuni hiyo ilisema itandelea kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine wa elimu kufanikisha elimu kusonga mbele na kutengeneza wanafunzi bora wanaosoma masomo ya sayansi hasa kuelekea ukuaji wa uchumi wa viwanda.

Naye Diwani wa kata ya Bonyokwa, Tumike Malilo, aliishukuru kampuni hiyo kuwaletea vifaa hivyo ambavyo vitasaidia walimu kukaa na kufanya kazi zao za ufundishajji katika mazingira mazuri.

Kabla ya kupokea vifaa hivyo, walimu walikuwa wanatumia viti na meza za wanafunzi.

Naye mwanafunzi wa kidato cha pili katika shule hiyo, Veronica Thomas, alishukuru kampuni ya halotel kwa kuwasaidia.

"Nashauri wazazi na walezi wawaruhusu wanafunzi wajiunge na Halostudy ili kuboresha elimu yao," anasema.

# Wataalamu uhamasishaji chanjo Uviko-19 watakiwa lugha nzuri

**Na Mary Geofrey,** ARUSHA

WATAALAMU wanaotekeleza Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili wa Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19, wametakiwa kutumia lugha nzuri kuelimisha jamii badala ya kutumia vyeo kutisha wananchi.

Wito huo ulitolewa jana jijini hapa na mtalaamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Profesa. Antony Keya, wakati akiwasilisha mada ya uzoefu katika uhamasishaji na utoaji wa chanjo kwa wataalamu wanaotekeleza mpango huo.

Profesa Keya aliwataka kutumia lugha nzuri ili kuwashawishi wananchi kukubali kuchanja badala ya kutumia mamlaka zao.

Pia, aliwataka watalaamu hao, kujua kwanini wananchi hawakubali kuchanja ili kuwaelimisha kwanza na kusaidia kubadilisha fikra zao.

"Tusitumie vyeo vyetu kutoa kauli za vitisho ili watu wachanje, tutumie lugha nzuri ili tueleweke. Msikimbilie tu kuwahamasisha wananchi wachanje bali mnatakiwa mjue kwanza sababu zinazowafanya wasichanje, ndipo muanze kuwapa elimu ya kina ya chanjo," alisema Profesa Keya.

Aliwataka wasibague makundi ya kuwapa elimu, lakini pia watumie maneno mazuri ya kifamilia kama dada, kaka, baba au mama. Profesa Keya aliwataka wataalamu hao pia wavae uhusika wa wananchi wakati wa kutoa elimu badala ya kujiona wanawazidi kila kitu.

Aliwahimiza pia kuwapa moyo wananchi na kuwaonyesha umuhimu wao katika kupata chanjo na faida zake.

Naye Daktari Mshauri wa Magonjwa ya Ndani na Maradhi ya Moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), akichangia mada katika semina hiyo, alisema changamoto kubwa ya wananchi inayowafanya washindwe kuchanja ni kuamini hakuna UVIKO-19.

Alisema zitafutwe njia mpya za kuelezea dalili za UVIKO-19 kulingana na mabadiliko ya aina ya kirusi badala ya kutumia dalili za awamu za kukohoa, mafua na kuumwa kichwa.

Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili wa Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19 unatarajiwa kuzinduliwa leo mkoani hapa.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Mkoa wa Kigoma, Jumanne Tenganya, akiwasilisha hoja za kiutumishi kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa (hayupo pichani), wakati wa ziara ya kikazi ya waziri huyo ya kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa miradi ya TASAF katika mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Agizo 'seal' kwenye chupa latekelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

AGIZO la serikali kusitisha utengenezaji na uwekaji wa plastiki laini (seal) kwenye mifuniko ya chupa za maji limeendelea kutekelezwa tangu lilipotolewa Oktoba 11, mwaka huu, na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa ziara ya Waziri Jafo kufuatilia maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na serikali kuhusu utunzaji wa mazingira.

Alitembelea na kukagua Kiwanda cha Watercom kinachozalisha maji ya Afya na cha Tanzania Ruidar Co. Ltd kinachojishughulisha na urejelezaji plastiki na kuzalisha mabomba vilivyoko eneo la Kisarawe II katika Manispaa ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Jafo alisema serikali ilitoa maelekezo hayo kutokana na seal hiyo kutorejelezeka na inachafua mazingira pindi inapotupwa na kuzagaa ovyo, hali inayosababisha vifo vya mifugo na samaki baharini wanapoimeza.

Waziri huyo alibainisha kuwa pamoja na maelekezo hayo ya serikali, bado kuna baadhi ya kampuni hazijatekeleza huku akisisitiza kuwa ifikapo tarehe ya mwisho ya marufuku hiyo maji yatakayokuwa yanaendelea kuwekewa seal hiyo, yatapigwa marufuku sokoni.

Vilevile, aliwatoa wasiwasi wananchi wanaodhani kuwa bila matumizi ya vifaa hivyo, kuna uwezekano wa maji kuchakachuliwa, akisema kuwa matumizi ya mhuri wa moto yatasaidia kuondoa shida hiyo.

"Nimekuja hapa kwenye kiwanda hiki cha maji na nimefarijika sana kuona tayari wameshaanza kutekeleza agizo hilo, hawaweki tena viplastiki vile na wanatumia mtambo maalumu wa kuweka mhuri na huyu ametambua umuhimu wa kulipa kodi. Kwa hiyo, huwezi kununua maji hayo hadi yawe na mhuri huo," alisema.

William Mhavila kutoka kitengo cha uzalishaji cha kampuni hiyo alisema hivi sasa wanatekeleza agizo la serikali kwa kusitisha uzalishaji wa vifuko hivyo.

"Kama mnavyoona tumezima mtambo huu uliokuwa unazalisha zile seal za plastiki na hivyo tumeanza kutekeleza agizo la serikali ili tuweze kutunza mazingira," alisema Mhavila.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo alizuru katika kiwanda cha Tanzania Ruidar Co. Ltd kinachojihusisha na urejeleshaji wa plastiki na kuzalisha mabomba.

Akiwa kiwandani huko, alionyesha kuridhishwa na utekelezaji wa agizo lake la miezi mitatu kwa kampuni hiyo la kurekebisha mfumo wa uchujaji wa majitaka ambao ulitiririsha majitaka kwenye makazi ya watu. Waziri Jafo alisema kiwanda hicho kimetekeleza agizo hilo kwa asilimia 100 na kuwataka wengine waige mfano huo kwa mustakabali wa kulinda mazingira.

Pia alielekeza maofisa mazingira kufuatilia viwanda mbalimbali katika eneo hilo la Kigamboni kuona namna wanavyotimiza matakwa ya kisheria katika utunzaji wa mazingira.

Meneja wa kiwanda hicho, Zhang Ping, alisema kutokana na hatua hiyo, hivi sasa anarejeleza majitaka tofauti na awali alikuwa akinunua mara kwa mara, hivyo kupunguza gharama.

# Tarime yatoa mil. 148/- mikopo riba nafuu

Na Samson Chacha, TARIME

VIKUNDI 32 vya makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu Halmashauri ya mji Tarime, vimepokea mikopo isiyo na riba ya Sh. 148,000,000.

Mikopo hiyo ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri ambayo hutolewa kwa vikundi vya wajasiriamali wakiwamo vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kutekeleza agizo la serikali.

Akitoa hundi yenye thamani ya fedha hizo, Desemba 16, mwaka huu, Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mtenjele, alisema serikali inahimiza halmashauri zote kupitia makusanyo ya mapato ya ndani, kutoa asilimia 10 kwa ajili ya kuwapa mikopo vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

"Tunampongeza Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa serikali yake kuwajali wajasiriamali kwa kutoa mikopo isiyo na riba kwa ajili ya kuwainua kiuchumi na kimaendeleo, mikopo hii mnatakiwa kuitumia vyema kwa malengo mliojiwekea yaliyokusudiwa kuwainua kiuchumi," alisema na kuonya isitumike kwenye starehe za sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

Alisema, takwimu zinaonyesha kinamama wanaongoza katika urejeshaji wa mikopo hiyo ikilinganishwa na vijana na watu wenye ulemavu.

"Tunawapongeza kinamama kwa kurejesha mikopo mnayopewa kwa wakati ili muweze kukopa mingine na kwa vijana na wenye ulemavu rejesheni mikopo kwa wakati ili vijana wenzenu nao waweze kukopeshwa na kujiinua kimaisha," alisema Kanali Mtenjele.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji, Vitus Gwanko, alisema halmashauri imetoa kiasi hicho cha fedha kutoka makusanyo ya ndani kati ya hizo Sh. 101,000,000 ni fedha za marejesho kutoka vikundi hivyo na Sh. 47,000,000 ni makusanyo ya ndani.

Alisema kuna vikundi 14 kati ya 32 vikiwamo vya vijana na wenye ulemavu ambavyo vinasuasua kurejesha mikopo yao ambavyo vimeandikiwa barua na kusudio ni kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Gimbana Ntavyo, alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 halmashauri ya mji imetoa mikopo kwa makundi maalumu ya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu Sh. 148,000,000 na kuwahimiza wajasiriamali waliopata mikopo kutumia vyema kwa maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla ili kujiinua kimaendeleo.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, akizungumza na viongozi wa Wilaya ya Handeni juzi, wakati akikabidhiwa vyumba viwili vya madarasa vilivyojengwa kwa fedha za Uviko-19 katika Shule ya Sekondari Kwamatuku wilayani humo, (kushoto) ni Mkuu wa Wilaya hiyo Siriel Nchembe. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Wadau elimu wafundwa udhibiti ubora

Na Gideon Mwakanosya, SONGEA

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Caroline Nombo, amewataka waratibu elimu kata, wakuu wa shule za sekondari na walimu wakuu wa shule za msingi nchini kuzingatia mafunzo waliyopatiwa ya udhibiti wa ubora wa elimu.

Prof. Nombo aliyasema hayo juzi mjini hapa wakati akifunga mafunzo ya udhibiti ubora wa elimu kwa wakuu na waratibu hao katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Alisema mafunzo hayo ambayo yamefanyika nchi nzima kwa malengo ya kutaka mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu, yatachochea kupanda kwa taaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kwamba kwa wahitimu yatawapa nguvu na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Prof. Nombo aliwataka wahitimu hao kujitathmini juu ya ufundishaji na utoaji wa elimu kabla ya kufanyiwa tathmini na watu wengine katika uboreshaji, usimamizi na uendeshaji wa shule.

Naye Mratibu wa Mafunzo Mkoa wa Ruvuma ambaye pia ni Ofisa Mdhibiti Ubora wa Shule za Msingi na Sekondari Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Zephania Japhet, alisema mafunzo hayo yalishirikisha washiriki 11,580 kwa nchi nzima na kwa mkoa wa Ruvuma walikuwa 584.

Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Elimu, Ephrasia Buchuma, aliwahimiza washiriki wa mafunzo hayo kuona umuhimu wa kusimamia watoto ambao walikumbwa na changamoto mbalimbali zilizowafanya washindwe kuendelea na masomo pamoja na suala la utoaji wa adhabu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Steven Ndaki, aliipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuona umuhimu wa kutoa mafunzo ya udhibiti ubora wa elimu kwa walimu nchini na kuwataka wahitimu kuzingatia ubora wa elimu, ufundishaji na kuwataka kuwa jicho katika sekta ya elimu.

Mwenyekiti wa Mafunzo hayo, Abdallah Mchelu, akizungumza kwa niaba ya washiriki wenzake, aliishukuru serikali kupitia wizara kwa kuwapatia mafunzo hayo ambayo alisema yataleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu nchini.

# DC aanzisha kampeni utatuzi kero wananchi

Na Steven William, IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ameahidi kuzitafutia ufumbuzi kero mbalimbali zinazowagusa wananchi kuanzia ngazi ya kijiji ndani ya wilaya hiyo.

Moyo alitoa ahadi hiyo juzi alipokuwa akisikiliza kero za wananchi katika ziara yake ya kikazi katika vijiji vya Malinzanga, Mafuruto na Nyamahanga iliyombatana na ukaguzi vyumba 66 vya madarasa ya sekondari ambavyo vimefikia hatua ya mwisho ya ujenzi.

Alisema ziara ya kikazi ya kusikiliza kero za wananchi aliyoipa jina la 'Ulipo Nipo' inaendelea na mpaka sasa ameshawafikia wananchi kusikiliza kero katika vijiji 103 kati ya vijiji 134.

Moyo alisema amekuwa akitembea vijiji mbalimbali na kuelezwa kero mbalimbali na kwamba baadhi ameshazipatia ufumbuzi kwa kushirikiana na viongozi wenzake wakiwamo madiwani, kamati ya ulinzi na usalama na wakuu wa idara za halmashauri.

Kwa sasa, alisema hivi sasa anaendelea na ziara katika vijiji vilivyobaki kwa ajili ya kusikiliza kero kama ambavyo aliteuliwa kwa lengo la kupata kero na kuzitafutia ufumbuzi kwa kushirikiana na viongozi wenzake ndani ya wilaya.

Alisema kero ambazo ziko ndani ya uwezo wake na viongozi wengine ndani ya wilaya wanazishughulikia na zile zinazohitaji ufumbuzi kutoka juu, wanaziwasilisha katika ngazi ya mkoa na taifa.

Katika hatua nyingine, alisema kuwa katika Wilaya ya Iringa wanajenga vyumba vya madarasa 66 katika shule za sekondari na shule shikizi 28 na kwamba baadhi ya shule ujenzi umefikia hatua za mwisho kwa kuweka madirisha ya vioo.

Alisema wakati wowote kuanzia sasa, mafundi watakabidhi vyumba hivyo kwa kuwa ujenzi umefikia hatua za mwisho baadhi ya sekondari na zile shule shikizi.

Katika ziara hiyo, Moyo alikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari za Nyerere, Nyang'oro, Furahia, Kiwale, Ilambilole, Isimani na za shikizi za Kibaoni, Kigasi na Ikengeza.

# Ukatili kijinsia unavyorudisha nyuma jitihada Serikali kufikia uchumi wa juu

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye, amesema kuongezeka kwa vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto kunarudisha nyuma jitihada za serikali kufikia uchumi wa juu kutokana na jamii kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu madhara yake.

Andengenye aliyasema hayo akifungua kongamano la Kampeni ya 'Twende pamoja Kupinga Ukatili wa Kijinsia' lililofanyika mkoani hapa.

Alisema ili kufikia malengo ya kuwa na uchumi wa juu, unaotegemea viwanda ni muhimu kuwapo na ustaarabu ikiwamo kuheshimu utu wa mtu.

"Hata tukiendelea kujenga reli, shule, hospitali katika mahali ambapo utu wetu unadhalilishwa na kundi moja dhidi ya kundi lingine, vitu vyote hivyo vitakuwa havina maana," alisema Andengenye.

Kadhalika, alisema uchumi utakuwa wa maana kama utaonyesha ustaarabu na ustawi wa watu wanaonufaika na uchumi huo kwa kukemea vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto ili vitokomezwe kabisa.

"Ukatili hasa wa kijinsia una madhara makubwa hata kufikia wanawake kutoshiriki shughuli za ujasiriamali na tunafahamu hapa Kigoma nguvu kazi kubwa ni wanawake hivyo nguvu hii lazima ilindwe kwa nguvu zote," alisisitiza.

Alikumbusha kuwa iwapo jamii inataka watoto wasome, wawe na afya njema na maadili ni lazima kuanza mapambano ya kuwalinda wanawake na watoto kwa nguvu zote ili kupata wataalamu wa hapo baadaye.

Alisema sababu za vitendo vya ukatili ni ukosefu wa elimu katika jamii kuhusu jinsi na jinsia, mila na desturi kandamizi pamoja na umaskini hali inayosababisha utumikishwaji wa watoto na kulazimishwa kuolewa katika umri mdogo.

Andengenye alisema Kampeni ya Twende pamoja inamgusa kila mwananchi kwa kuwa ukatili unafanyika katika maeneo mbalimbali kuanzia nyumbani, shuleni, maeneo ya wazi na kazini na wakati mwingine unafanywa na watu walioaminiwa.

"Ni jukumu letu sote kuhakikisha tunatoa taarifa ya matukio ya ukatili na unyanyasaji kwa wanawake na watoto katika mamlaka za serikali na polisi na kuhudhuria katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa wakati. Hakuna jambo rahisi ambalo tunarithisha kwa vizazi vijavyo kama ukatili. Katika hali yoyote ukatili ukifanyika tusipoukemea tujue kizazi kitakachokuja kitakuwa na uwezo na nguvu zaidi wa kufanya ukatili kuliko sisi."

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magwiza, akiwasilisha lengo la kongamano hilo, alisema tangu mwaka 2018 serikali ilipozindua MTAKUWWA, lengo lilikuwa kupunguza ukatili kwa wanawake na watoto kwa asilimia 50, lakini kupitia mijadala hiyo itasaidia kupunguza zaidi idadi hiyo.

# Wakulima wakumbwa hofu mifugo kula chumvi 'feki'

**Na Thobias Mwanakatwe,** NGORONGORO

ZAIDI ya wafugaji 8,000 wa kata za Ngorongoro na Nainokanoka, wamekumbwa na hofu ya ng'ombe wao kupoteza maisha baada ya kupewa chumvi iliyochanganywa na mawe na rangi inayosababisha wanapoitumia uharisha.

Chumvi hiyo ambayo imezua utata inadaiwa imesambazwa kwa wafugaji hao na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ikiwa ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mwaka 2016.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo kwa NCAA iwe inawapa wafugaji chumvi ya kulisha mifugo pamoja na maji ili wafugaji waache kupeleka mifugo yao ndani ya Bonde la Ngorongoro ambako walikuwa wakifuata chumvi ya asili na maji katika bonde hilo ambayo inasaidia sana kwa afya za mifugo.

Hata hivyo, wafugaji wamelalamika kuwa chumvi waliyopewa wiki mbili zilizopita haina viwango na imechanganywa na mawe na rangi na mifugo yao inapotumia inaharisha hali ambayo inahatarisha afya ya ng'ombe hao.

Diwani wa Kata ya Ngorongoro, Simon Saitoti, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili alisema hali sio nzuri kwa mifugo ya wafugaji wa kata hiyo baada ya kuitumia chumvi hiyo ambayo inadaiwa kununuliwa na NCAA kutoka nchi jirani.

Saitoti alisema katika kata yake ililetwa mifuko 900 na ilikuwa imeshasambazwa kwa wafugaji zaidi ya 5000 na kubaki sita pekee kupitia kwa wenyeviti wa vijiji na baada ya ng'ombe kuanza kuitumia wakaanza kuona dalili tofauti.

Alisema baada ya kupelekewa malalamiko na wafugaji naye alitoa taarifa kwa Ofisa Mifugo na viongozi wa NCAA na kulitishwa kikao cha wenyeviti wa vijiji vya Kayapusi, Oloilobi na Mokilale ambacho pia kilihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala.

Saitoti alisema mfuko mmoja wa chumvi hiyo wenye ujazo wa kilo 20 walipochanganya kwenye maji walibaini kuwapo kwa mchanga na rangi ambayo ilipakwa mchanga huo hali ambayo imetia shaka ya usalama wa mifugo ya wafugaji ambayo tayari imeshatumia chumvi hiyo.

Naye Kaimu Mhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Elibariki Bajuta, alipoulizwa kwa njia ya simu kuhusu suala hilo alikiri NCAA kupokea malalamiko ya wafugaji kuhusu chumvi hiyo ambayo kila mwaka imekuwa ikisambazwa na mamlaka kwa wafugaji wa kata tatu za wilaya ya Ngorongoro.

"Malalamiko tumeyasikia, ni vitu vya kawaida tu tatizo limetokea, hii chumvi inayolalamikiwa tuliisambaza mwishoni mwa mwezi uliopita (Novemba)," alisema Bajuta alipopigiwa simu.

Kwa upande wake mtaalamu wa mifugo wa NCAA, Kilasi Mollel, alipoulizwa alisema kama jambo hilo limejulikana shirika (NCAA) italifanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Mangwala alisema juzi (Jumatatu) alifika eneo la tukio katika Kata ya Ngorongoro na kuzungumza na wafugaji na kutoa agizo chumvi hiyo isiendelee kutolewa kwa wafugaji tena na wale ambao wamekwishapewa wasiipe mifugo.

Mangwala alisema hatua nyingine iliyochukuliwa na serikali ni kuchukua sampuli ya mfuko mmoja wa chumvi hiyo inayodaiwa kuwa feki ili ipelekwe kwa Mkemia Mkuu wa Serikali ufanyike uchunguzi wa kisayansi. Alisema majibu ya uchunguzi huo yatakapotoka wafugaji watajulisha nini cha kufanya.

Utaratibu wa kutoa chumvi bure kwa wafugaji wa kata za Ngorongoro na Nainokanoka ulianza kutekelezwa mwaka 2017 baada ya serikali kupiga marufuku wafugaji kupeleka mifugo yao 'Ngorongoro crater'.



Katapila likisawazisha eneo ambalo awali lilikuwa likitumiwa na wafanyabiashara wadogo, Mbezi Mwisho Dar es Salaam juzi, ambapo kwa sasa wameondolewa na kupelekwa katika masoko. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Makamba aipa REA mbinu nishati mbadala

**Na Veronica Simba**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amewaelekeza viongozi na wafanyakazi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kuongeza nguvu katika aina nyingine za nishati kama inavyofanyika kwenye umeme.

Alisema REA imeendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa usambazaji nishati ya umeme vijijini ni vyema pia ikifanya hivyo katika aina nyingine za nishati zenye matumizi makubwa zaidi, husussan zinazotumika kupikia.

Waziri Makamba alikuwa akizungumza na wafanyakazi wa REA ili kutoa dira na mwelekeo wa wizara yake, ikiwa ni mara ya kwanza kukutana nao rasmi juzi tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo. Alisema wengi wanaitafsiri REA kuhusika na nishati ya umeme pekee kutokana na kuweka nguvu nyingi kwenye nishati hiyo, na kwamba ni muhimu kwa wakala huo kuzipa uzito unaostahili nishati nyinginezo ambazo ni jukumu lake pia.

Akitoa mfano, Waziri Makamba alieleza kuwa utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa kwa Tanzania, matumizi makubwa ya nishati yako majumbani. Aidha, aliongeza kuwa nishati inayotumika zaidi majumbani hususan katika kupikia ni tungamotaka.

Alisema, asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini na wanatumia nishati ya tungamotaka katika kupikia. "Nataka mfanye mabadiliko kwenye nishati ya kupikia maana ndiyo inagusa Watanzania wengi zaidi," alisisitiza.

Pia, aliitaka REA kuimarisha kitengo chake cha utafiti na kianze mara moja kufanya utafiti mbalimbali utakaoleta mapinduzi makubwa katika sekta ya nishati, husussan vijijini.

"Mathalani, kuna mawazo au fikra gani mpya ya kuwasaidia Watanzania wapate nishati safi ya kupikia? Je, nishati ya kupikia ina mchango gani katika kuongeza au kupunguza gharama za maisha? Hizi ni baadhi ya tafiti zinazopaswa kufanyika," alisisitiza Makamba.

Katika hatua nyingine, alitoa maagizo kuwa makandarasi wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini, wanapobainika kufanya udanganyifu kwenye miradi hiyo, wachukuliwe hatua kali ikiwamo kuondolewa na kutopewa fursa ya kufanya kazi hizo.

Vilevile, washtakiwe kwa mamlaka zote husika pamoja na kufanya ufuatiliaji ili wasipewe kazi nyingine katika eneo lolote ili iwe fundisho kwao kwa kuwaumiza wananchi na kuliingizia hasara taifa. Pamoja na maelekezo hayo, Waziri aliipongeza REA kwa kazi nzuri inayofanya na kuitaka kuongeza juhudi zaidi katika kuwatumikia Watanzania.

Alisema kuwa serikali inajivunia utendaji kazi wa REA na ni mojawapo ya taasisi zinazotegemewa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa REA, Mhandisi Hassan Saidy, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu kwa waziri, alisema kazi kubwa imefanyika na hadi sasa upatikanaji umeme vijijini umefikia asilimia 69.6.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Nishati Vijijini, Wakili Julius Kalolo, akizungumza kwa niaba ya Bodi, alimhakikishia waziri kuwa maelekezo yote aliyoyatoa yatafanyiwa kazi.

# Wasafirishaji haramu wa binadamu kukiona cha moto

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga, imewataka wananchi wanaojihusisha na vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu kuacha mara moja, huku ikiagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuwasaka na kuwafikisha mahakamani watakaobainika kufanya biashara hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alitoa kauli hiyo jana wakati wa kikao cha kutoa elimu kwa maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama mkoani hapa, kwa ajili ya kupambana na tatizo la usafirishaji haramu wa binadamu kilichofanyika wilayani Kahama chini ya Taasisi ya Tanzania Relief Initiatives.

Mjema alisema, suala hilo ni janga kubwa la taifa na serikali haiwezi kuendelea kulifumbia macho kwa kuwa linawezekana kukomeshwa endapo kila mwananchi ataonyesha ushirikiano wake kwa kutoa taarifa za usafirishaji wa binadamu na kuwachukulia hatua wanaofanya vitendo hivyo.

"Hili ni wimbi linakuja nchini na kuanza kuwashawishi vijana wetu na kuchukuliwa na kupelekwa kusikojulikana kwa madai ya kwenda kufanyakazi, tusikubali haya yakaanza kutokea mkoani kwetu tuchukue hatua kwa kupinga na kutokomeza biashara hii," alisema Mjema.

Kwa upande wake, Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, Salum Rashidi, alisema, wengi huwa wanasafirishwa kwa kutumia vyombo vya usafiri wa abiria tofauti na kipindi cha nyuma kwenye magari ya mizigo.

Pia alisema kwa sasa kuna mtindo mpya ambao wasafirishaji wamegundua kusafirisha binadamu watano katika magari ya abiria, lakini huwa wanafanya msako na kuwabaini na kuwachukukulia hatua ikiwa ni kuwafikisha mahakamani.

Naye Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, ACP George Kyando, aliwataka viongozi wa dini kuhakikisha wanatoa angalizo kwa waumini wao wakati wa ibada ili kutojihusisha na vitendo vya usafirishaji haramu wa binadamu na kuwasihi kutoa taarifa endapo wataviona vitendo hivyo.

"Wengi waliokuwa wakifanya biashara hii walidhani kwamba kumsafirisha binadamu mwenzie si kosa...Sasa awe amekubali kusafirisha au amekataa hata kama tunafahamu wapi unampeleka tukikukamata lazima tukuchukulie hatua," alisisitiza ACP Kyando.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Tanzania Relief Initiatives, Edwin Mugambila, alisema vijana wanarubuniwa na watu wenye nia ovu kwa kuwapatia kazi za ndani, elimu nzuri huku wengine wakiahidiwa kwenda nje ya nchi kwa madai ya kufanyakazi zenye malipo mazuri.




Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga bidhaa zao licha ya kuwekewa bango katika eneo la Kimara Mwisho, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Diwani aomba serikali ujenzi bweni kuokoa wanafunzi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

DIWANI wa Ubena Halmashauri ya Chalinze, Geofrey Kamugisha, ameiomba serikali kujenga bweni katika Sekondari ya Ubena, kuokoa wanafunzi wanaopata mimba na wengine kukatisha masomo kutokana na umbali.

Aliyasema hayo juzi mjini hapo kuwa kushuka kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kinachangiwa na umbali wa shule kwa baadhi yao kushindwa kumudu kutembea.

Alisema vijijii vya Visakazi, Tukamisasa na Kaloleni, kata ya Ubena baadhi ya wanafunzi wa kike wamekatisha masomo kwa kupata mimba ambazo zimesababishwa na shule kuwa mbali na makazi.

"Kuna wanafunzi wanakatisha masomo kwa mimba, wapo pia walioacha shule kwa utoro sugu, hii ni kutokana na madhara ya ukosefu wa bweni kwenye shule," alisema.

Alisema, wanafunzi wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 20 kwenda na kurudi nyumbani kila siku.

Alisema kuwa katika Kijiji cha Tukamisasa, wazazi wanalazimika kuwapangishia watoto nyumba katika maeneo ya Ubena Zomozi ambako huishi bila tahadhari na usimamizi wa kutosha wa wazazi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, alisema halmashauri hiyo inajipanga kuondoa vikwazo katika sekta ya elimu ili kuinua ufaulu.

**"Kuna wanafunzi wanakatisha masomo kwa mimba, wapo pia walioacha shule kwa utoro sugu, hii ni kutokana na madhara ya ukosefu wa bweni kwenye shule," alisema. Alisema, wanafunzi wanalazimika kutembea umbali wa kilomita 20 kwenda na kurudi nyumbani kila siku.**

# MNH kuanza upandikizaji uloto nchini

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa kushirikiana na Hospitali ya Saratani ya Healthcare Global Enterprises (HCG), wanashirikiana kutoa huduma za upandikizaji uloto kwa wagonjwa wa saratani ya damu nchini.

Katika ushirikiano huo, wataalamu kutoka HCG wanawaongezea uwezo wataalamu wa afya wa MNH ili waweze kuwahudumia wagonjwa wa magonjwa ya damu nchini. Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Damu na Upandikizaji wa Uloto kutoka Hospitali ya Saratani ya HCG ya Bengaluru India, Dk. Sachin Jadhav, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ushirikiano huo juzi, alisema mafanikio katika mpango huo yamechangiwa na mafunzo shirikishi na kubadilishana maarifa baina ya pande hizo mbili.

"Kwa kushirikiana na MNH tumefanya upandikizaji wa uloto ambao ni chembe-hai mama, kutoka sehemu moja ya mwili kwenda nyingine, ulifanyika kwa wagonjwa watano wenye miaka kati ya miaka 34 hadi 55 waliokuwa na saratani ya damu ambayo kwa jina la kitaalamu hujulikana kama Myeloma.

"Katika ugonjwa huu, upandikizaji wa chembe-hai mama unaweza kuongeza umri wa kuishi kwa takribani mara mbili na pia huimarisha hali ya mgonjwa," alisema.

Alisema ushirikiano huo, unaenda sambamba na dhamira ya India ya kuendelea kuisaidia Tanzania katika kutengeneza mfumo unaojitegemea wa huduma za afya na kurahisisha upatikanaji wa huduma bora za matibabu kwa Watanzania bila kusafiri nje ya nchi.

Alisema kituo chao kipya cha kupandikiza uloto kitashughulikia ufanyaji wa vipimo na tathmini za wagonjwa kabla ya kufanya upandikizaji, matibabu ya kemotherapia kabla ya upasuaji, upandikizaji wa chembe-hai, pamoja na ufuatiliaji wa muda mrefu baada ya upandikizaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, alishukuru kwa ushirikiano huo ambao utasaidia hospitali hiyo kutoa huduma bora kwa wagonjwa katika hatua zote za matibabu.

"Upandikizaji wa uloto, sasa unaweza kufanyika kwa gharama nafuu tofauti na hapo awali, mgonjwa alilazimika kutumia takribani Sh. milioni 250 nje ya nchi, lakini kwa sasa mtu atalipa Sh. milioni 70 hapa MNH na hivyo kuokoa zaidi ya Sh. milioni 180.

"Hii inaleta matumaini mapya kwa wagonjwa wa saratani. Tuna bahati kubwa kupata kituo hiki kwa msaada wa wataalamu bobezi kutoka Hospitali za Saratani za HCG kutoka India," alisema Prof. Museru.

Pambazuko jipya upinzani baada ya mkutano wa vyama
Ukurasa 12



Ukurasa 14






BAADA YA KONGAMANO LA VYAMA

# Wachambuzi waiambia serikali dai la katiba mpya halikwepeki

**Na Sabato Kasika**

SIKU chache baada ya mkutano wa Msajili wa Vyama vya Siasa na wadau wa siasa kupitisha maazimio 80 katika kongamano lililofanyika Dodoma wiki iliyopita, wachambuzi wa siasa wanayaangazia baadhi ya maazimio hayo na kusema hitaji kuu linabaki kuwa katiba mpya.

Miongoni mwa maazimio hayo ni suala la katiba mpya na tume huru ya uchaguzi, ambapo wadau wameazimia kuwa badala ya kuendelea na mchakato wa kusaka maoni ya kuandika katiba mpya, yachaguliwe mambo machache yanayolalamikiwa sana na kuanza kuyafanyia kazi.

Aidha, kwenye suala la tume huru ya uchaguzi, mkutano huo umeazimia kuwa wadau waongeze imani kwa viongozi na watendaji wa tume hiyo, huku wakitaka suala la rushwa kwenye uchaguzi kufanyiwa kazi kwa umakini ili kuikomesha.

Wadau hao wamekubaliana kufanyika kwa mapitio ya sheria ya vyama vya siasa, mchakato uwe shirikishi na pia kupitia Sheria ya Jeshi la Polisi ili liwe na weledi na kuondoa uonevu unaofanywa kwa kisingizio cha kutekeleza sheria.

Lakini pia, wamekubaliana kufuata katiba, sheria, kanuni na miongozo katika kutekeleza majukumu yao, na kwamba vyombo vya maamuzi vina wajibu wa kutenda haki na kulinda amani, kwa kuwa msingi wa amani ni haki.

Kwa baadhi ya maazimio hayo waliyoyataja, suala la katiba mpya na tume huru ya uchaguzi zimekuwa vikipewa uzito na wadau wa siasa nchini wakiamini kwamba vikipatikana vinaweza kusaidia vyama ya upinzani kufurukuta na kuondokana na kilio hicho wanachokitoa kila mwaka.

Hata hivyo, katika mkutano huo, vyama vya NCCR -Mageuzi na CHADEMA, havikuhudhuria, kila kimoja kikiwa na sababu zake, lakini CUF, ACT- Wazalendo na vingine vidogo vilihudhuria.




Rais Samia Suluhu Hassan alipofungua mkutano wa wadau wa siasa. **PICHA: MTANDAO**

Baada ya kutolewa maazimio hayo, Nipashe inazungumza na wachambuzi na wadau wa siasa kwa ajili ya kupata maoni yao jinsi wanavyoyachukulia baada ya mkutano huo na hasa suala la kuandikwa katiba ya wananchi na tume huru ya uchaguzi.

**KATIBA MPYA KWANZA**

Mjumbe wa Baraza la Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Hebron Mwakagenda, anasema, hakuna nchi ambayo ina katiba ya kudumu, hivyo kuweka viraka ni jambo la kawaida, lakini hitaji la katiba mpya lipo na lipewe nafasi.

Mchambuzi huyo wa siasa anasema, mabadiliko yatakayofanywa kwenye katiba kama ambavyo wadau hao wamekubaliana, yazingatie yale yaliyopendekezwa na Tume ya Jaji Warioba.

"Hakuna nchi imewahi kuwa na katiba inayojitosheleza, hivyo kwa uamuzi wa kutaka kuanza na mambo yanayolalamikiwa, ni hatua nzuri lakini hitaji la katiba mpya ni kubwa zaidi," anasema Mwakagenda.

Anaongeza kuwa katiba iliyopo ni kama inapendelea chama kimoja hali ambayo inasababisha malalamiko, na kwamba marekebisho yakifanyika yatakuwa yamegusa hadi tume huru ya uchaguzi. "Sidhani kama wapinzani wanaweza kuwaamini watendaji na viongozi wa tume hiyo, kutokana na jinsi ambavyo wamekuwa wakiwakwamisha katika uchaguzi hata kwa vitu vidogo," anasema

Mwakagenda na kukumbusha kuwa maazimio yanaweza kuwa zaidi ya 80, na kwamba, msingi mkuu ni katiba ambayo ni sheria mama ikiwa imebeba matarajio ya watawaliwa na watawala kwa maendeleo ya nchi yao, hivyo isifumbiwe macho.

**NI KATIBA TU**

Maggid Mjengwa ni mchambuzi wa siasa, ambaye anasema, maazimio hayo ni mazuri, lakini anaamini mchakato wa katiba mpya ungepewa nafasi ya kipekee, kwa maelezo kuwa ingemaliza kasoro zote zilizopo sasa.

"Katiba mpya ni muhimu sana, hasa ikizingatia mapendekezo ya Tume ya Jaji ya Warioba ingawa mchakato wake haukwenda vizuri bungeni baada ya baadhi ya wadau kuususia," anakumbusha Mjengwa.

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa Tume ya Jaji Warioba ilizingatia haki za binadamu, kwa maelezo kuwa haki ndiyo msingi mkuu wa amani, ambayo anasisitiza kuna umuhimu wa kuendelea na mchakato wa kuipata.

Anasema, ni wakati sasa wadau wote kukaa pamoja na kuanzisha mchakato wa kupatikana kwa katiba yenye maslahi kwa pande zote kwa madai kwamba pesa nyingi zimetumika kukusanya maoni na hata Bunge Maalum la Katiba.

"Katiba mpya ni madai ya muda mrefu ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi, hivyo wameazimia kufanya marekebisho kwa yale yanayolalamikiwa sana, ni muhimu serikali na wadau wa siasa kukutana na kujadiliana jinsi ya kufikia hatua ya kupata katiba mpya," anasema.

**VIRAKA SASA BASI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kiota Women Health and Development (KIWOHEDE), Justa Mwaituka , anasema viraka havifai katika katiba na kwamba pamoja na maazimio ya mkutano, anataka kilio cha wengi kisikiwe.

"Kilio cha wengi ni katiba mpya siyo kuweka viraka, hivyo kwa maoni yangu ni kwamba, ingawa muda ni mfupi kufikia uchaguzi wa 2025 bado inaweza kupatikana kama kuna nia ya kweli," anasema Mwaituka.

Anafafanua kuwa ni muumini wa rasimu ya Jaji Warioba, na kwamba alishiriki kutengeneza bunge la watoto kutoa mawazo yao kwenye rasimu hiyo katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Mtwara, Kigoma na Dar es Salaam, hivyo umuhimu wake unabakia palepale.

"Turudi kwenye rasimu ambayo ilikuwa imeshirikisha wadau mbalimbali kwani ilionyesha uongozi unavyotakiwa kuwa ikawa imetengenisha vizuri mihimili mikuu mitatu ya dola na kuainisha jinsi ya utendaji kazi wake," anasema.

Justa anaeleza kuwa rasimu hiyo pia iliainisha jinsi ya kukuza utawala bora demokrasia na namna ya kupata tume huru ya uchaguzi na jinsi ya kujikimu kibajeti kwa maendeleo ya Tanzania na watu wake. "Ni suala la utashi wa kisiasa tu kufikia uamuzi wa kuwa na katiba mpya, na ninaamini kwamba penye nia pana njia, hivyo ni muhimu kusikia kilio cha wengi ili wapate katiba wanayoitaka siyo yenye viraka," anasema.




Zito Kabwe Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo. **PICHA: MTANDAO**

# Pambazuko jipya upinzani baada ya mkutano wa vyama

**Na Ani Jozeni**

TANZANIA inatembea katika mazingira ya kutafakari nini cha kufanya ili iendelee, kwa maana ya kuhakikisha maendeleo ya uchumi, uthabiti wa nchi na mtangamano kisiasa miongoni mwa raia unadumishwa.

Hautakuwa mtihani rahisi kwani wale wanaojadili wanaegemea upande mmoja, wa kuwapo kwa uhuru wa kukusanyika na kufanya siasa kama katiba inavyotaka.

Upande wa pili, unaotoa tahadhari, ni ule wa dola, na haielekei kuwa itakuwa rahisi kueleza kwa umakini ulazima wa kuzuia uhuru wa kukusanyika, kutoa maoni kwani washiriki hawatakuwa wameona kuna tatizo gani kuendelea na mfumo huru kisiasa kama hapo mwanzo.

Ndivyo anavyosema mwanasiasa mwandamizi Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, anapohudhuria kongamano la vyama vya siasa la wiki iliyopita lililofunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Hapo kuna mtego wa kisiasa, kwani hata wakati ule ushiriki wa vyama vya upinzani haukuwa unakwenda moja kwa moja na kile dola inachotaka, yaani siasa za kistaarabu ambazo hazina vurugu na kejeli zisizovumilika kwa walio madarakani.

Anachotaka serikali ni kuwa kanuni ambazo dola inataka zikubaliwe na vyama vya upinzani, na siasa za wazi zikianza tena, kusiwe na haya ya kufungia vyama.

Licha ya kuwa Rais Samia ameonyesha dhamira ya wazi ya kurudisha siasa za vyama vingi kushamiri, hapana shaka kuwa anataka mwelekeo wa baadhi ya vyama na hasa kile kikuu cha upinzani cha CHADEMA unabadilike.

Japo hakukitaja kwa jina lakini tangu Chama cha Wananchi (CUF) kilipofikia baada ya uchaguzi mkuu wa 2005, ni CHADEMA ambayo imekuwa mstari wa mbele kiupinzani na kupata idadi kubwa ya wabunge na uungwaji mkono.

Uchaguzi wa hivi karibuni, kuanzia wa serikali za mitaa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu 2020 iliwekwa

> Licha ya kuwa Rais Samia ameonyesha dhamira ya wazi ya kurudisha siasa za vyama vingi kushamiri, hapana shaka kuwa anataka mwelekeo wa baadhi ya vyama na hasa kile kikuu cha upinzani cha CHADEMA ubadilike.

pembeni kibabe, baada ya kunyamazishwa kwa muda mrefu hadi uchaguzi ulipokaribia; uliendeshwa 'Kiafrika' dola likiwa na uhakika ni nani anatakiwa ashinde, takriban katika majimbo yote.

Tuseme unaweza kuanzia hapo katika kujadili mustakabali wa vyama vingi nchini, na nini hasa kinatakiwa kufanyika ili hatima ya nchi na maendeleo visivurugwe na uendeshaji wa mfumo wa vyama vingi.

Swali jingine ambalo unaweza kuuliza ni iwapo chama tawala kinaweza tena kuruhusu mfumo halisi wa vyama vingi, uendeshwe kwa hisia za viongozi wa vyama tofauti, na siyo kwa kufuata mwelekeo kama unavyotakiwa na dola.

Hapo labda kuna angalizo kuwa wakati viongozi wa CCM kwa ujumla wao wanapendelea vizuizi vilivyoko dhidi ya upinzani, uongozi wa nchi unataka uhuru, ila unabanwa kuhakikisha kuwa uhuru hauchochei siasa za vurugu ambazo baadhi wanajua zinafaa zaidi.

Kusema kuwa uchaguzi mkuu wa 2020 na ule wa serikali za mitaa kabla yake uliendeshwa 'Kiafrika' ni dhana halisi ya kitaaluma badala ya ile ya kiitikadi, kuwa uchaguzi huo ulikuwa wa kibabe na hakuna zaidi ya hapo.

Kuendesha uchaguzi Kiafrika ni kutoruhusu upinzani kutetemesha dola, hasa pale ambako dola hiyo inaungwa mkono katika mapana na marefu ya nchi, licha ya upinzani kuishi na hofu, kama ilivyokuwa awamu ya tano.

Taifa lilikuwa linajua kuwa wapinzani wanaishi kwa hofu ila siyo wao tu; ni pamoja na wakubwa serikalini waliozoea kutenda watakavyo, wasiulizwe chochote.

Suala hapa ni kuwa wakati mfumo wa vyama vingi ulipewa sifa kubwa kuanzia mwaka 1992 uliporudishwa enzi ya awamu ya pili, uliokuwa unayazungumzia kama kuondoa ufisadi serikalini, kukiuka maadili ya uongozi na kutokuwajibika ipasavyo, yalifanyiwa kazi na kuleta 'usafi' katika uongozi wa umma na awamu ya Rais John Magufuli kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, akitumia falsafa ya kutumbua majipu na kupambana na mafisadi.

Kimsingi mfumo huo sasa wa kuubana upinzani unawafurahisha wana-CCM kote nchini, na unaweza kusema hitaji lake linaonekana kwani baadhi ya maofisa wanachotoka ni kufanya watakavyo. Bila kuwa na jicho la kuwabana na kuwadhibiti matokeo yake ni rushwa kusambaa, uonevu kuimarishwa kila mahali.

Jambo ambalo baadhi ya wanaharakati katika kongamano hilo walielekea kusahau ni kuwa wanaona mikataba ya Umoja wa Mataifa kuhusu uhuru wa mtu binafsi na hivyo uhuru wa vyombo vya habari na vyama vya siasa ndiyo msingi wa majadiliano.

Ingekuwa ni hivyo wangekuwa na 'kete' zote upande wao, kuwa kinachongojewa ni kuvielekeza vyombo vya usimamizi wa shughuli za kisiasa kufuata katiba, huku sheria zinazopigiwa kelele kama ile ya Msajili wa Vyama vya Siasa na ile ya Jeshi la Polisi zikifanyiwa marekebisho, kama wanaharakati walivyosisitiza katika jumuisho la mapendekezo muhimu au matazamio yao kuhusu kuendeleza demokrasia nchini.

Kibano halisi ambacho kitawaoongoza wakuu wa dola katika kuchuja mapendekezo ya upinzani na wadau wa mfumo wa vyama vingi ni dukuduku katika ngazi za CCM na wananchi kwa jumla kuwa kwa kuziweka pembeni mbinu au nyenzo za utawala za awamu ya tano, nchi 'inaharibika.'

Wanaangalia utendaji serikalini na ufanisi huduma za jamii ambako 'baadhi ya wakubwa' wakiachiwa tu wananchi watalipishwa kila kitu, kwa michango na faini zinazopangwa na watawala serikalini.

Hivyo kizuizi kikuu cha mfumo halisi wa vyama vingi ni kuwa unawasitiri walio serikalini kutenda watakavyo, na wapinzani kuleta vurugu. Hali hiyo ikianza kuwa ya kawaida kuelekea uchaguzi mkuu ujao, upinzani ndani ya CCM unaweza kuanzisha rasmi 'plan B.'

# Dk. Mwinyi anavyobeba bango la kuwa 'Rais bora mwaka 2021'

**Na Deogratias Mutungi**




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: MTANDAO**

MWANAFALSAFA nguli Plato, katika maandiko na machapisho yake aliwahi kuelezea sifa za uongozi, akisema ni nani anafaa kuwa kiongozi na yupi asiyefaa kuongoza. Alifafanua kuwa kiongozi sharti awe na uwezo mkubwa wa utambuzi na utatuzi wa mambo, awe na elimu ya kutosha, busara na hekima.

Ndiyo aliowaita "wafalme wa falsafa' (philosopher kings). Dhana ya uwezo mkubwa wa utambuzi na utatuzi wa mambo kisiasa, kupata muafaka na kuanzisha upya maisha kwa raia bila kujali itikadi zao visiwani Zanzibar, inalandana na falsafa ya wanaofaa kuwa na viongozi, inayotajwa na Plato.

Rais Dk. Hussein Mwinyi wa Zanzibar, anavyowaongoza Wazanzibari leo anaweza kufananishwa na shujaa wa Afrika Nelson Mandela, aliyetumia falsafa za unyenyekevu kisiasa, maono na busara kumaliza sintofahamu kati ya pande zinazokwaruzana.

Kisiasa kiongozi anayesimamia miiko na maadili, katiba na sheria na utawala bora anaaminiwa kuwa ni mkomavu kisiasa aidha amepikwa na mifumo na ameandaliwa kuwaongoza watu na rasilimali.

Mwinyi kama Mandela alipikwa na kuiva kisiasa kadhalika, utashi wake wa mapinduzi ya sera, siasa na uchumi wa Zanzibar kwa awamu ya nane siyo suala la bahati bali mkakati na mipango ya kimfumo iliyomtengeneza kiweledi.

Uongozi bora na ushujaa wa Rais Mwinyi Zanzibar unaanzia kwenye uthubutu, busara na umakini wa kuongoza, amethubutu, amefanya na kwa kipindi cha muda mfupi ameweza kuwaunganisha Wazanzibari licha ya utofauti wa kiitikadi na kuwa "philosopher king" anayezungumziwa na Plato.

Rais Mwinyi, amewezaje kufanikisha utengamano huo wa kisiasa baina ya CCM na chama kikuu cha upinzani, Zanzibar ACT-Wazalendo, ambao kihistoria wafuasi wake wengi walitoka CUF baada ya kutofautiana na Mwenyekiti Profesa Ibrahim Lipumba na Katibu Mkuu Maalim Seif Sharif Hamad (marehemu).

Historia inaonyesha na kusimulia uhasama baina ya wafuasi wa vyama hivyo uliokuwa mkali, uliojenga visasi, chuki na mauaji. Kwa mfano yaliyotokea Januari 26 na 27, 2001 na vurugu nyingine za chaguzi.

Rais Mwinyi amewezaje kurejesha matumaini mapya ya utengamano wa amani si siri ni kutumia uongozi makini, ametumia busara, hekima na ukomavu wa kisiasa kutafuta amani ya kudumu miongoni mwa Wazanzibari ikiwa ni pamoja na busara za ushawishi wa kushirikiana na vyama vikuu vya upinzani ndani ya serikali.

Agenda ya Rais Mwinyi ipo wazi na inajitambulisha bayana kisiasa kuwa ni kujenga umoja wa kitaifa kwa maslahi ya jamii ya Wazanzibari wote.

Mbali na kuisimamia ipasavyo katiba ya Zanzibar, tafakuri ya kisiasa inaonyesha Mwinyi amechagua maridhiano ya amani ili kuujenga uchumi wa Zanzibar kwa maslahi ya wote.

Kauli mbiu isiyokuwa rasmi ya awamu ya nane ya uchumi na maendeleo kwanza, mengineyo baadaye na kinachofanywa na Rais Mwinyi ndicho Mandela alichosimamia mwaka 1994 kujenga Afrika Kusini kiuchumi.

Alisimama na kila mmoja akasimamia mifumo ya ustawi wa maendeleo ya Waafrika Kusini akijua kuwa kati ya sababu nyingi za umaskini wa Afrika mojawapo kujenga chuki za kisiasa na visasi zisizokuwa na tija.

Huo ndiyo ushuhuda unaoonekana Ethiopia katika Jimbo la Tigray na kwingineko ni ombwe la uongozi wa Kiafrika katika kupambania kuhodhi himaya na madaraka, ambavyo Biblia inautaja kama ubatili mtupu (kujilisha upepo).

Miongo kadhaa, tawala nyingi za Kiafrika kisiasa zinakosa viongozi wenye falsafa na maono kama ilivyo kwa Rais Mwinyi wa Zanzibar, hali hiyo ilisababisha Afrika kujikuta ikitawaliwa kimabavu na mkono wa chuma, udikteta, kunajisi katiba na kuminya demokrasia kwenye mifumo ya vyama vingi vya upinzani.

> "Huo ndiyo ushuhuda unaoonekana Ethiopia katika Jimbo la Tigray na kwingineko ni ombwe la uongozi wa Kiafrika katika kupambania kuhodhi himaya na madaraka, ambavyo Biblia inautaja kama ubatili mtupu (kujilisha upepo).

Badala ya kuunganisha wananchi kujenga taifa, viongozi huzalisha matabaka ya chuki baina ya watu, vikundi na jumuiya mbalimbali kwa maslahi yao binafsi kwa faida ya maangamizo ya taifa. Kwa uthabiti uliopo sasa na hatua za maendeleo zilizofikiwa na serikali ya awamu ya nane ya SMZ kwa kipindi cha mwaka mmoja, Rais Mwinyi anaweza kusimikwa kuwa ni kiongozi bora ambaye ameonyesha umahiri katika utawala na uongozi wenye tija.

Ni kwenye maisha ya watu wa kawaida, kwenye uchumi wa Zanzibar na Bara, kama Afrika ingekuwa na viongozi mahiri kama Dk. Mwinyi, ingekuwa imepiga hatua kubwa kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kimaendeleo kwa kuwa maelewano, upendo na kuheshimiana ndiko kunakoleta maendeleo.

Viongozi bora wenye maono, dira na falsafa za ukombozi wa kiuchumi baada ya ukombozi wa bendera kati ya miaka ya 1957-1994, hauna maana kama hakuna taasisi imara za kuleta maendeleo ambazo ni uongozi thabiti.

Kinachoendelea Zanzibar kwa sasa chini ya Rais Mwinyi ni uongozi unaoacha alama wenye mantiki na utashi wa kuongoza watu kwa mafanikio yao kwa lengo la kugusa maisha ya kila mwananchi wa kawaida na kumwinua kiuchumi na kimaendeleo.

Kuongoza kwa mabavu kufisidi rasilimali na demokrasia pamoja au kujenga hofu dhidi ya wananchi ili waiogope dola na serikali yako, siyo mwelekeo sahihi.

Leo ni kuongoza kwa dira yenye fursa sawa kwa wote, kanuni ambazo alizitumia Mandela kuiongoza Afrika Kusini chini ya ANC (African National Congress), iliyoandaa mazingira ya Afrika Kusini moja.

Kwa zama za sasa unapoongelea utawala wa alama na unaoacha urithi "legacy" kwa watawala wa Afrika huwezi kukosa kulitaja jina la Rais Mwinyi wa Zanzibar, kwa kipindi kifupi ameonyesha uwezo na umahiri wa kuongoza kwa vitendo kwa kile alichokiahidi wakati wa kuomba ridhaa ya kushika dola na kuisimamia ilani ya CCM.

Viongozi wengi wa kisiasa wabadilike na kuachana na kushindwa kutimiza ahadi zao kwa wapiga kura waliowachagua, aidha watawala wengi waache kukengeuka baada ya kushika dola.

Enzi za Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU) mwaka 1967, Kwame Nkrumah Rais wa zamani wa Ghana, aliwahi kumwambia Mwalimu Julius Nyerere "dola ni tamu sana na hukengeusha watawala hivyo tujitahidi kuunganisha Afrika na Waafrika kama nchi moja kabla hatujanogewa zaidi na kiti cha urais."

Jiulize nini kilifata? Jibu ni hili hadi sasa imebakia kuwa ndoto kuiunganisha Afrika kuwa taifa moja, mantiki hapa ni kuwa viongozi wengi hupofushwa na madaraka na kukengeuka kisiasa, ili kulinda maslahi yao.

Kwa kutumia usemi wa 'jenga daraja na si kuta,' falsafa za kisera, kimfumo na utashi wa kisiasa wa serikali ya sasa ya awamu ya nane ya Dk. Mwinyi Zanzibar, linalojengwa ni daraja la kudumu la ustawi wa mustakabali wa Wazanzibari wote.

Katika fursa za amani, uchumi na maendeleo ya kweli, Zanzibar ya sasa imenoga kisera, kiutendaji na kimkakati ukuta wa uhasama umevunjwa rasmi na sasa Zanzibar ni moto katika uwajibikaji na usimamizi bora wa rasilimali za nchi.

Ni wazi kuwa siasa imara ni zao la ustawi wa amani na maendeleo ya watu, ni chemichemi na kiungo cha utaifa wa mtu na mtu, siasa mbovu ni chanzo cha matatizo na mifarakano inayohatarisha utu na uhai wa binadamu.

Aidha, bila siasa safi na uongozi bora ni vigumu kuwapo na upendo na umoja wa kitaifa katika mifumo ya uzalishaji mali na kiuchumi.

***Maoni: dmutungid@yahoo.com.***

# RAIS ADAMA BARROW

- Aliwahi kuwa 'sungusungu' London
- Licha ya kula kiapo cha urais ugenini
- Wagambia wampa ushindi wa kishindo




Rais Adama Barrow, baada ya kushinda uchaguzi mkuu mwanzoni mwa Desemba. **PICHA: DW**

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

ADAMA Barrow ni Rais wa sasa wa Gambia. Hivi karibuni ameshinda katika uchaguzi mkuu uliofanyika Desemba 6, 2021.

Ana sifa kubwa ya kumtoa ikulu ya Banjul mbabe Yahya Jammeh, aliyeiongoza nchi hiyo kwa miongo miwili ya ukandamizaji wa demokrasia. Safari hii Barrow anaibuka tena kidedea kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika wiki ya kwanza ya Desemba, 2021 na kuandika historia ya kuendeleza demokrasia ya uchaguzi huru, wa haki na unaokubalika.

Ushindi wa Barrow ulioshangiliwa na umati wa wafuasi wake alipowahutubia kwa hali ya furaha na unyenyekevu mkubwa na kuwataka wafuasi wake kuwaheshimu waliowapigia kura wapinzani wake katika uchaguzi aliouita kuwa huru, wa haki na wa uwazi.

"Ninawaomba wafuasi wangu wote kusherehekea ushindi kwa njia ya amani. Tunakumbushwa kwamba waliotaka kuunga mkono wagombea wengine ni Wagambia na haki yao ya kufanya hivyo lazima iheshimiwe daima," anasema Barrow.

Kwa mujibu wa DW, Barrow apata ushindi mkubwa ambaye baada ya kuchukua kiti cha urais miaka mitano iliyopita aling'oa miaka 20 au miongo miwili ya udikteta kwenye taifa hilo. Rais huyo alipata zaidi ya asilimia 53 ya kura, kama ilivyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Gambia na mpinzani wake mkuu Ousainou Darboe, akishika nafasi ya pili kwa kuzoa asilimia 27.7.

Kwa mujibu wa DW, uchaguzi huo wa kwanza tangu dikteta wa zamani Yahya Jammeh kukimbilia uhamishoni, unaonekana kuwa muhimu kwa demokrasia changa ya Afrika Magharibi.

**ALIPOCHAGULIWA 2017**

Barrow anaingia kwenye uongozi wa taifa hilo kwa mara ya kwanza 2016, akimbwaga Jammeh na kuwa rais mpya wa Gambia, akianzisha awamu ya tatu.

Baada ya uchaguzi Adama Barrow, aliapishiwa nchini Senegal wakati viongozi wa Afrika wa Jumuiya ya Uchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) walipomshawishi kiongozi aliyekuwapo madarakani dikteta Jammeh ajiuzulu.

> "Ninawaomba wafuasi wangu wote kusherehekea ushindi kwa njia ya amani. Tunakumbushwa kwamba waliotaka kuunga mkono wagombea wengine ni Wagambia na haki yao ya kufanya hivyo lazima iheshimiwe daima," anasema Barrow.

Wanadiplomasia walimtaka Barrow arudi mara moja nyumbani kuepuka pengo la uongozi, lakini licha ya kurejea nyumbani, hali haikuwa salama kwenye ikulu ya Banjul. Kiongozi huyo alilazimika kuishi katika makazi yake, wakati ikulu ikifanyiwa ukaguzi na uchunguzi, kuangalia kama kuna hatari baada ya kuondoka kwa Yahya Jammeh.

Jammeh aling'ang'ania kukaa ikulu kabla ya kwenda uhamishoni Guinea ya Ikweta na kabla ya Barrow kuingia Gambia, baada ya kula kiapo ugenini, vikosi vya wanajeshi wa mataifa ya Afrika Magharibi viliweka ulinzi mkali nchini humu kukabiliana na vikosi vitiifu kwa Jammeh.

**ALIKUWA 'SUNGU SUNGU'**

Mwanasiasa Adama Barrow alizaliwa mwaka 1965 katika kijiji kimoja karibu na mji wa kibiashara wa Basse mashariki mwa Gambia, katika kutafuta maisha alihamia jijini London miaka ya 2000 ambapo anaripotiwa alifanya kazi kama mlinzi kwenye duka moja, kaskazini mwa London.

Ni katika kusaka pesa ili aendelee na masomo yake. Alirejea nchini Gambia mwaka 2006 ambapo alianzisha kampuni yake ya kuwekeza inayohusisha majengo na ardhi (real estate).

Kiongozi huyo mwenye miaka 56, aliteuliwa kuongoza muungano wa vyama saba vya upinzani kumpinga Rais Yahya Jammeh.

Baada ya kuingia madarakani 2016 alikosoa kutokuwapo kwa kipengele cha mihula ya uongozi katika katiba kwa urais na pia kulaani kufungwa kwa wanasiasa wa upinzani.

Ni kiongozi anayeunga mkono uhuru wa mahakama, wa vyombo vya habari na wa vyama vya kihiari.

**MGOMBEA HURU**

Barrow aliporejea Gambia 2006 alichaguliwa kuwa mweka hazina wa Chama cha United Democratic Party (UDP) na baadaye alichaguliwa kuwa kiongozi wake Septemba 2016, baada ya mkuu wa chama hicho kutupwa gerezani na serikali ya Jammeh.

Barrow aliteuliwa kuwa mgombea wa UDP katika uchaguzi wa Rais wa 2016, hata hivyo, baadaye zilitolewa taarifa kuwa anasimama kama mgomba huru lakini anayeungwa mkono na upinzani, ukifahamika kama 'Opposition Coalitions 2016 ukihusisha vyama vya UDP na vingine sita.

Katika uchaguzi huo alipata asilimia 43.34 ya kura za urais na kumbwaga mkongwe wa ikulu Jammeh, ambaye awali alikubali kushinda, lakini akaanza figisu na kutishia hatma ya rais mpya, hatua iliyomlazimisha Barrow kukimbilia Senegal.

Hata hivyo, dunia na Afrika ilipinga hatua hiyo na kulazimika kuingilia kati huku Wagambia wakibakia na sintofahamu ya nani atakuwa kiongozi wao.

Juhudi zilifanyika Barrow akaapishwa kwenye ofisi za ubalozi wa Gambia zilizoko Senegal mnamo Januari 19, 2016 na kuwa rais, huku Jammeh, akikimbilia Guinea ya Ikweta, siku tatu baadaye, hatua iliyompa Barrow nguvu ya kurejea nyumbani.

Katika harakati za kisiasa Adama Barrow ni kiongozi wa upinzani anayeibuka kutoka kwenye muungano wa upinzania nchini Gambia, katika uchaguzi wa 2016 alitangazwa kuwa mshindi wa uchaguzi wa urais akipata kura 263,515 huku Rais Yahya Jammeh akiambulia kura 212,099.

Kwenye uchaguzi huo wapiga kura wapatao 800,000 walijitosa kuchagua viongozi kwenye taifa hilo dogo la Afrika Magharibi.

Mstaafu Yahya Jammeh ambaye aliitawala Gambia kwa miaka 22 baada ya kuingia madarakani kwa njia ya mapinduzi alikataa kushindwa, licha ya baadaye kukubali kuondoka ikulu kwa shingo upande.

**KUNG'OKA JAMMEH**

Dikteta Jammeh aliingia Ikulu ya Banjul mwaka 1994 baada ya kufanya mapinduzi ya kijeshi yaliyomwondoa Rais wa kwanza wa taifa hilo, Sir Dawda Jawara. Tangu wakati huo dikteta huyo aliendelea kujipa ushindi mara tatu kila ulipofanyika uchaguzi na kuendeleza siasa za kibabe na ukandamizaji.

Sir Dawda Jawara, Rais wa kwanza wa Gambia na baba wa taifa hilo aliiongoza nchi hiyo tangu kupata uhuru miaka 1960 kutoka Uingereza, alifariki mwaka 2019 na kushuhudia mpinzani wake Yahya Jammeh akiondolewa ikulu na upinzani.

**MITANDAO**



# RC aweka msimamo kuhusu machinga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amesema serikali haitawavumilia machinga ambao watakutwa wamezagaa mitaani, barabarani na maeneo yasiyo rasmi kufanya biashara baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Machinga Open Market.

Aidha, amesema serikali pia italazimika kutumia nguvu za dola kuwaondoa wale wote watakaokaidi kwa kuvunjiwa vibanda vyao.

Mtaka alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na machinga kwenye hafla ya utiaji saini wa mkataba wa mradi wa ujenzi wa Machinga Open Market unaojengwa eneo la Bahi Road, jijini hapa.

Ujenzi huo unaofanywa na kampuni ya Mohamed Builders Limited kwa gharama ya Sh. bilioni 7.5 utakaokamilika Aprili, mwakani, machinga 2,938 watakuwa kwenye eneo hilo.

Mtaka alisema serikali itakuwa tayari kutumia dola kwa ajili ya kuwaondoa kwa nguvu wale wote watakaokutwa wakifanya biashara zao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.

Alisema lengo la serikali mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji ni kuwategulia kitendawili cha eneo la wafanyabiashara ambacho kitawafanya kuwa huru bila kubugudhiwa.

Kwa mujibu wa Mtaka, soko hilo litakuwa la kisasa ambalo litatumika kwa saa 24, kukiwa na ulinzi na usalama wa kutosha zikiwamo huduma za kibenki.

"Hivyo kukamilika kwa mradi huo hatutaki kuona biashara holela mitaani na zikionekana tutalazimika kuvunja na kusafisha, wakati eneo tayari limeshakamilika kwa ajili yenu," alisema Mtaka.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema halmashauri imeandaa eneo hilo kwa maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amezitaka halmashauri kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo.

Mafuru alisema kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa wa Dodoma, Halmashauri ya Jiji imetenga eneo la Bahi Road yalipokuwa yanaegesha malori ya mizigo kwa ajili ya machinga.

Alisema Jiji linajenga mradi huo wa soko kwa fedha za mapato ya ndani na zingine kutoka serikali kuu ambapo linatarajia kupata mapato yake kiasi cha Sh. bilioni 1.1 kwa mwaka.

# Kampuni za nje kufanya miradi ya REA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeandaa utaratibu mpya wa kushirikisha kampuni kubwa za umeme kutoka nje ya nchi ili kutekeleza miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa haraka na ufanisi kuliko ilivyo sasa.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, alibainisha hayo jana jijini Dodoma, alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa REA.

Makamba alisema serikali kupitia wizara yake inapanga kubadilisha utaratibu wa kufanya miradi ya REA ili kuongeza kasi ya utekelezaji na ufanisi.

"Hivi sasa utekelezaji wake utegemea fedha za mwisho wa mwezi hatuwezi kusubiri hadi miaka 25 ijayo kukamilisha miradi hii. Tunapanga kualika kampuni kubwa duniani zinazoweza fanya miradi mikubwa ya umeme.

"Kampuni kutoka nchi kama vile China ambako kuna kampuni zimefanya miradi ya umeme eneo kubwa kuliko hata Tanzania kwa haraka na ufanisi, lakini zingine ni kutoka Brazil ambao pia waliwahi kuwa na shida kama yetu," alisema Makamba.

Pia alisema serikali imepanga katika kipindi cha miaka minne ijayo kuwa imekamilisha kufikisha umeme katika vitongoji vyote 37,000 nchini vilivyobakia.

"Vitongoji 37,000 vimebaki kati ya vitongoji 64,000 nchini tunaweza kuvimaliza ndani ya miaka minne bila kusubiri fedha za mwisho wa mwezi kwa kushirikisha makandarasi ambao watakuja na fedha na sisi kuweka usimamizi kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

"Tunaweza kukubaliana na mkandarasi na kumpatia vitongoji 6,000 na tukaweka usimamizi mzuri tutapiga hatua kuliko ilivyo sasa. Nategemea kabla ya mwisho wa Januari, mwakani, tutawaeleza nini tunataka kufanya na kwa uharaka zaidi. Hii habari ya nguzo imeanguka, transifoma feki tunaachana nayo," alisisitiza Makamba.

Aidha, waziri huyo aliutaka uongozi wa REA kusimamia taratibu na miongozi ya sheria ya ununuzi wa umma ambayo imekuwa ikilalamikiwa na watu wengi katika wakala huo.

"Suala la kuzingatia utaratibu wa ununuzi unatia doa wakala. Naomba muuweke sawa tusijefika sehemu tukaonana wabaya. Haiwezekani suala la mtu kupata tenda REA waziri nasumbuliwa na watu kutaka niwape upendeleo. Mimi mambo haya sijazoea, naomba utaratibu huu muu-'fix' kabla hatujaonana wabaya. Nawataka, nawaelekeza, nawasihi suala hili tulitazame vizuri litawatia doa na tukifika huko hatutakuwa na mswalia mtume," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Bodi ya REA, Julias Kalolo, alimshukuru waziri kwa kutenga muda wa kuzungumza na watumishi wa wakala kwa mara ya kwanza toka ashike wadhifa huo.

Hata hivyo, alimwahidi kuwa yote ambayo amewaelekeza watayafanyia kazi kwa maendeleo ya taasisi hiyo na taifa kwa ujumla.




Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe (katikati), akitia saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa machinga Open Market unaojengwa eneo la Bahi Road na Kampuni ya Builders Limited juzi, (kushoto) Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Taher Jafferji, na (wapili kulia) Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Watanzania wahamasishwa ulaji nyama

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

KAMPUNI ya Ranchi za Taifa (NARCO), imehamasisha Watanzania kufuga kisasa na kibiashara mbuzi na kondoo ili kukidhi mahitaji ya soko la kigeni na viwanda vya nyama nchini.

Aidha, imetoa punguzo la bei msimu wa sikukuu ili kuhamasisha wananchi kula nyama ya mbuzi na kondoo na kupanua wigo wa soko la ndani.

Meneja Masoko wa NARCO, Mnzava Immanuel, alitoa rai hiyo jana wilayani hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Prof. Peter Msofe.

Alisema kuna umuhimu sasa Watanzania wakafuga mifugo hiyo kisasa ili kukidhi mahitaji ya soko na machinjio yaliyoko na viwanda vinavyoendelea kujengwa.

Kuhusu punguzo la bei, Mnzava alisema wamefikia hatua hiyo ili kuimarisha afya za Watanzania ambapo mbuzi 3,000 na kondoo 1,000 aina ya Blackhead Persian (BHP) watauzwa kwa bei ya punguzo la asilimia 33.

Alibainisha kuwa punguzo hilo litakuwa katika Ranchi za Kongwa, Ruvu, Mkata, Kalambo, West Kilimanjaro na Missenyi.

"Takwimu zinaonyesha kwamba ulaji wa nyama ya mbuzi na kondoo bado uko chini nchini ikilinganishwa na ulaji wa nyama ya ng'ombe ambao unaongezeka kila mwaka," alisema.

Hata hivyo, alisema mahitaji ya nyama ya mbuzi na kondoo katika soko la nje na katika machinjio na viwanda vya nyama vilivyoko na vinavyoendelea kujengwa nchini yanaongezeka, hivyo kutoa fursa ya soko hilo kwa wafugaji.

"Ofa hii ya Krismasi na Mwaka Mpya itatolewa kuanzia Desemba 21, hadi Januari 10, mwakani katika ranchi zilizotajwa katika ofa hii," alisema. Naye Meneja wa Ranchi ya Kongwa, Elisa Binamungu, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanatoa huduma kwa wananchi watakaojitokeza kuchangamkia fursa hiyo.

"Pamoja na ofa hii kila siku katika ranchi yetu tuna chinja ng'ombe kuna nyama nzuri, tunahamasisha wananchi katika kipindi hiki wakaribie waje wapate huduma sahihi kulingana na mahitaji yao," alisema.

Alisema nyama hiyo ina ubora wa tofauti na mifugo ya kawaida kutokana na kupitia utaratibu wa unenepeshaji.



# Wataka zahanati ya kijiji kupandishwa hadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Shizuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuipandisha hadhi zahanati ya kijiji cha Shisyete kuwa kituo cha afya.

Wananchi hao walitoa ombi hilo wakati wa makabidhiano ya miundombinu mbalimbali iliyojengwa na serikali kwa ushirikiano na Shirika la SAWA chini ya ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF).

Mmoja wa wananchi hao, Salome Shega, alisema zahanati hiyo imekuwa ikitoa huduma bora za matibabu ikiwamo huduma ya wajawazito kujifungua, lakini kwa wanawake wanaojifungua kwa mara ya kwanza wamekuwa wakilazimika kwenda kujifungulia kituo cha afya.

Alisema kituo cha afya kilicho jirani ni cha Ilembo ambacho kiko umbali wa kati ya kilomita sita na saba, hivyo wengi wanahofia maisha yao hali ambayo alisema imepunguza hata kiwango cha wananchi kuzaliana kwenye kata hiyo.

"Tunaishukuru serikali pamoja na SAWA wametusaidia kuboresha zahanati yetu na sasa tunapata hata huduma za kujifungua hapa. Lakini bado tuna shida ya kituo cha afya hivyo tunamwomba mkurugenzi kama itampendeza atupandishie zahanati hii hadhi," alisema Shwenga.

Naye Mariam Jengela alisema kata hiyo ina maeneo mengi ya wazi, hivyo serikali ikiamua inaweza ikawasaidia kujenga kituo cha afya kipya, wako tayari kuchangia nguvu zao pamoja na eneo kwa ajili ya mradi huo.

Alisema zahanati yao baada ya kufanyiwa maboresho na SAWA, sasa hivi wanapata huduma nzuri hasa wanawake na watoto, lakini tatizo lililoko ni pale mtu anapopatiwa rufani kwenda kituo cha afya hasa nyakati za usiku na kipindi cha mvua.

Akiikabidhi serikali mradi huo, Mwakilishi wa SAWA, Joachim Asenga, alisema wamejenga matundu sita ya vyoo kwa ajili ya mahitaji mbalimbali kwenye zahanati hiyo pamoja na kuweka huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Asenga alisema wamejenga matundu saba ya vyoo ambayo matatu ni kwa ajili ya watumishi, matatu ni kwa ajili ya wagonjwa na moja ni kwa ajili ya wanawake waliojifungua ambao awali walikuwa wanalazimika kwenda nje kwenye vyoo vya wagonjwa.

Vyoo hivyo, alisema vimejengwa kwa kuzingati mahitaji mbalimbali yakiwamo ya watu wenye ulemavu pamoja na watoto ili makundi hayo yasichangamane na watu wengine.

"Kama mnavyojua UNICEF inashughulika na watoto kwa hiyo kati ya matundu matatu ya choo cha wagonjwa, moja ni kwa ajili ya watoto na iko hivyo kwa sababu watoto wanakuwa na magonjwa tofauti na watu wazima," alisema Asenga.

Alisema mbali na ujenzi wa miundombinu hiyo pia wamejenga eneo maalumu la wanawake waliojifungua kufulia nguo zao kwa madai kuwa awali walikuwa wanalazimika kurudi na nguo chafu nyumbani kwenda kuzifua.

Akipokea miundombinu hiyo kwa niaba ya serikali, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Yahya Msuya, aliishukuru UNICEF kwa msaada huo na kusema umesaidia kuboresha huduma za afya ndani ya halmashauri hiyo.

Alisema kabla ya zahanati hiyo kuboreshwa wanawake wengi walikuwa wanajifungulia nyumbani lakini baada ya kuboreshwa wengi wanajifungulia kwenye zahanati hiyo na kwamba mpaka sasa tangu ifunguliwe wanawake 32 wameshajifungulia hapo.



Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh Door Issa Mohamed (kushoto), akiwaongoza watumishi wa Jiji hilo kwenye kikao cha kujadili ushirikiano wa kimaendeleo kati ya Jiji hilo na Jiji la Zurishi nchini Uswizi mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Waziri ataka taasisi maji kushirikiana

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewataka watumishi wa taasisi mbalimbali zinazohusika na maji katika mkoa wa Songwe kushirikiana katika kuwahudumia wananchi ili kuhakikisha tatizo la huduma hiyo linabaki kuwa historia.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa anazungumza na watumishi wa idara hizo katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe.

Alisema hakuna sababu ya taasisi hizo kubaguana kwa sababu ya utofauti wa majukumu yao.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Mamlaka ya Maji Safi ya Usafi wa Mazingira Songwe, Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mabonde ya Maji ya Ziwa Rukwa na Mto Songwe pamoja na taasisi ya ubora wa maji ambazo alidai zinashughulikia kitu kimoja.

Waziri Aweso alisema isiwapo taasisi yoyote ya kukwamisha wananchi kupata maji kwa ajili ya matumizi huku akisisitiza kuwa serikali imekuwa ikiwaahidi wananchi kupata huduma hiyo muhimu na hivyo ikitokea wakakwamishwa inaweza kuwa tatizo.

"Mimi nawahakikishia kwamba wataalamu wa ofisi yangu hawatakuwa kikwazo kwa namna yoyote kwenu, lakini nanyi naomba msiwe kikwazo kwa wananchi mnaowahudumia kupata huduma ya maji, tuliwaahidi na tunatekeleza," alisema Aweso.

Alisema lengo la serikali kwa sasa ni kuhakikisha wananchi wengi wa mijini na vijijini wanapata maji ya bomba kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kutekeleza azma ya kumtua mama ndoo kichwani.

# Walia tembo kuvamia na kuharibu mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kata ya Igawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali iwasaidie kudhibiti tembo ambao wamekuwa wakivamia na kuharibu mazao.

Tembo hao wanaelezwa kuwa wamekuwa wakitoroka kutoka katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuingia kwenye vijiji hivyo ambavyo vinapakana na hifadhi hiyo hali ambayo pia inachochea uhusiano mbaya kati ya vijiji na hifadhi.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema wanyama hao wamekuwa wakisababisha hasara kubwa ikiwa ni pamoja na kuwafanya wakumbwe na njaa kwa kuharibu mazao yao hasa mahindi, mpunga, viazi na karanga.

Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Gaitan Madindo, alisema msimu uliopita kata hiyo ilivamiwa na kundi la tembo zaidi ya 100 na zaidi ya ekari zaidi ya 400 za mazao na hivyo kuwasababishia wananchi hasara kubwa.

Alisema wanyama hao wamekuwa wakiharibu mazao hasa nyakati za usiku wakiwa wamelala na kwamba hata wakiwaona huwa ni vigumu kuwadhibiti kutokana na kuogopa kudhurika.

Madindo alisema maofisa wa Hifadhi ya Ruaha wamekuwa wakitoa elimu ya kuwadhibiti, lakini inapotokea makundi ni makubwa wanashindwa kutumia mbinu hizo kupambana nayo na hivyo mazao kuvamiwa na kuharibiwa.

"Tunachomshukuru Mungu ni kwamba kwa sasa wanyama hawa hawajasababisha madhara kwa binadamu kutokana na watu wengi kuogopa kuwasogelea, mtu anaona ni bora awaache waharibu mazao lakini yeye awe salama," alisema Madindo.

Naye Sabini Mwailemi alisema unapotokea uharibifu wa mazao, fidia wanayolipwa na serikali huwa haiendani na gharama za uzalishaji, hivyo akaiomba serikali kubadili sheria inayosimamia fidia ili angalau ziwe zinapunguza machungu.

Alisema msimu uliopita baada ya tembo kuharibu mazao yao, maofisa wa TANAPA walifanya tathmini na kuwalipa Sh. 20,000 kwa ekari jambo ambalo liliwafanya wananchi kukata tamaa ya kuendelea kujishughulisha na kilimo.

Diwani wa Igava, Nasoro Udes, alisema kwa sasa maofisa wa TANAPA wameshawafundisha wananchi namna ya kutumia pilipili kuwazuia wanyama hao kuingia kwenye mashamba yao lakini hofu yao ni ufanisi wa mbinu hiyo.

Alisema shughuli kubwa za wananchi wa kata yake ni kilimo na kwamba ndiyo shughuli inayowaletea fedha pamoja na chakula, hivyo akaiomba serikali iwasaidie kulinda mazao yao.

Alisema wananchi wa kata hiyo wamekuwa wakishiriki pia kwenye shughuli za uhifadhi kwa kuhakikisha wanazuia majangili kuingia hifadhini pamoja na kutoingiza mifugo ndani ya hifadhi.

"Lakini sisi hatuwezi kuidhuru hifadhi kwa sababu na sisi ni wanufaika, tumekuwa tukishirikiana na maofisa wa hifadhi kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu," alisema Udes.

Mbarali ni miongoni mwa wilaya zinazopakana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na hivi karibuni maofisa kutoka katika Shirika la Taifa la Hifadhi za Taifa (TANAPA) waliamua kuanza kuwatumia wananchi kulinda hifadhi hiyo.



# Waasisi Mapinduzi kuenziwa kisheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuelekea miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, marekebisho ya muswada wa sheria ya kuwaenzi waasisi wa Mapinduzi ya mwaka 1964 unatarajiwa kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea hivi sasa.

Hayo yalisemwa jana katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Muhammed, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho na shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi.

Alisema tangu mwaka 1964 waasisi na viongozi hao wamekuwa wakienziwa na kuna wiki ya kumuenzi mwasisi wa Mapinduzi hayo, Abeid Amani Karume lakini kwa sasa wataenziwa kisheria tofauti na awali.

Waziri alisema serikali ya awamu ya nane chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Mwinyi, inakuja na mabadiliko hayo ya sheria ya kuwaenzi waasisi wa Mapinduzi kuenziwa kisheria.

"Serikali inakuja na mabadiliko ya kisheria ya kuwaenzi viongozi wakuu wa kitaifa walioshiri katika mapinduzi na sheria hiyo itajadiliwa katika kikao hiki cha tano cha Baraza la Wawakilishi ili viongozi walioshiriki katika Mapinduzi ya Januari 12, 1964 wawe wanaenziwa kisheria," alisema.

Pia alisema kilele cha maadhimisho ya miaka 58 yatafanyika Januari 12, mwakani, katika Uwanja wa Amani Mjini Zanzibar ambapo kutakuwa na gwaride rasmi kutoka kwa askari wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na burudani mbalimbali za ngoma za asili.

"Ili kuwapa fursa wananchi wa Zanzibar kushiriki maadhimisho hayo, serikali ya Zanzibar itawasafirisha wananchi 200 kutoka wilaya zote za Pemba kushiriki sherehe hizo," alisema.

Waziri alisema kabla ya kilele cha maadhimisho ya sherehe hizo kutakuwa na shughuli mbalimbali zikiwamo uzinduzi na uwekaji wa mawe ya msingi ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aliitaja miradi hiyo ni 30 ambapo 13 itaweka mawe ya msingi na 23 itazinduliwa ikiwamo ufunguzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu ya Zanzibar, Tunguu, ufunguzi wa kiwanda cha ushoni na kiwanda cha viatu cha kikosi cha Valantia na ufunguzi wa kiwanda cha nguo.

Kwa mujibu wa waziri, pia kutakuwa na tamasha la maonyesho la biashara litakaloanza Januari 8, mwakani, katika Viwanja vya Maisara mjini Zanzibar.

Wafanyabiashara mbalimbali kutoka Zanzibar na Tanzania Bara watashiriki maonyesho hayo.

Alisema pia kutakuwa na utoaji wa nishani ili kuenzi mchango uliotolewa na Wazanzibari mbalimbali katika maendeleo ya nchi katika utumishi wa umma na maeneo mengine na serikali itatoa nishani maalum ya Mapinduzi kwa watu watakaoandaliwa kupokea nishani hiyo.

Waziri huyo alisema maadhimisho hayo yatafungwa na fainali ya mpira wa miguu yatakayofanyika katika Uwanja wa Amani Januari 13, mwakani, ambapo kauli mbiu ya mwaka huu katika Miaka 58 ya Mapinduzi ni Uchumi wa Bluu kwa Maendeleo Endelevu.

## Serikali yakiri ongezeko mahabusi magerezani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amekiri kuwapo kwa msongamano wa mahabusi katika magereza Zanzibar.

Amesema ongezeko la mahabusi hao linatokana na tuhuma za makosa ya udhalilishaji na ubakaji ambayo hayana dhamana kwa sasa.

Haroun alisema hayo jana katika Kikao cha Bazara la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Uzini, Shaaban Ali Othman, aliyetaka kujua idadi kamili ya mahabusi walioko katika magereza ya Unguja na Pemba.

Alisema katika kutokana na msongamano huo, Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar na Mkurugenzi wa Mashtaka, walifanya ziara katika Chuo cha Mafunzo Kilimani Novemba, mwaka huu, na kuzungumza na wanafunzi hao (wafungwa) wanaokabiliwa na tuhuma mbalimbali.

Hadi sasa, alisema kuna wafungwa 166 na mahabusi 386 wanaosubiri uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka.

Hata hivyo, alisema katika ziara hiyo imebainika kwamba mahabusi wengi ni wale walioshtakiwa kwa udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji, mambo ambayo hayana dhamana.

Alisema kazi kubwa inayofanywa kwa sasa kupitia ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Jeshi la Polisi ni kuongeza kasi ya kufanya upelelezi wa tuhuma zinazowakabili ili kufikisha mashauri yao mbele ya mahakama.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Muhamed, akizungumza jana na waandishi wa habari ambao hawapo pichani kuhusu Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri ataka ushirikiano kuweka mji safi

**Na Rahma Suleiman,**
**ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, amewataka wananchi kuunga mkono jitihada za serikali katika kuhakikisha mji unakuwa safi.

Kufanya hivyo kutaisaidia Zanzibar kuwa na haiba nzuri ambayo itaweka ustawi bora na kivutio kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa mifuko maalum ya kuhifadhia taka na magari ya kisasa ya kusafirishia yaliyotolewa na Kampuni ya Vicline katika Uwanja wa Mapinduzi Square, Kisonge mjini Zanzibar.

Alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ametoa rai yenye dhamira njema kuhakikisha mji unakuwa safi, hivyo iko haja ya wananchi kushirikiana kwa pamoja kudumisha usafi katika maeneo yao.

Pia alisema kampuni ya Vicline itashirikiana na serikali kuondoa changamoto iliyoko ya kuzagaa kwa taka katika mji jambo ambalo linapoteza haiba na ustawi wa mji.

Alisema suala la kujenga nchi sio la serikali pekee bali ni jukumu la wananchi wote, hivyo iko haja ya ushirikiano ili kuhakikisha azma iliyokusudiwa inafikiwa.

Waziri Masoud alisema licha ya taka kuna uchafuzi wa mazingira ya kubandika matangazo mengi kiholela bila ya kufuata utaratibu kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, alisema bado mji haujaridhisha hasa katika mkoa huo ambao ni jicho la Zanzibar, hivyo sheria ndogo ndogo zipitishwe kwa kutoa faini kwa wanaochafua mji.

Alisema ni vyema jamii kuimarisha mji kwa kupanda bustani mbalimbali katika maeneo yao ili kutenengeza uzuri wa mji wa Zanzibar.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa Mjini, Ali Khamis, alisema Baraza la Manispaa kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa taka kumetokana na gharama kubwa ya uendeshaji, uchakavu na uwezo mdogo wa vifaa vya ukusanyaji wa taka pamoja na uchache wa rasilimali watu.

Mwenyekiti wa Vicline ambaye ni Mbunge wa Mpendae, Taufiq Salum Turky, alisema kampuni hiyo ina mkakati wa kuzisarifu taka kwa lengo la kubuni miradi na kuzalisha viwanda vidogo vya vyakula vya kuku, majongoo mbolea pamoja na karatasi jambo ambalo litasaidia kutoa fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Akitoa wito kwa jamii alisema usafi ni jukumu la wote hivyo tushirikiane tuimarishe mji kwa pamoja na kaulimbiu ya uzinduzi huo ya 'Weka Mji Safi kwa Utalii Bora Zanzibar'.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TANGAZO KWA UMMA

## UHUISHAJI WA LESENI ZA UZALISHAJI BIDHAA ZINAZOTOZWA USHURU WA BIDHAA / DENATURED SPIRITS

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wazalishaji na wanaotarajia kuanza uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo (denatured spirits) kuwa, leseni za mwaka 2021 zilizotolewa chini ya kifungu Na. 8 na/au 16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, zinatarajiwa kufikia ukomo wa matumizi mnamo tarehe 31 Desemba 2021. Hivyo basi, wazalishaji wanakumbushwa kuleta maombi kwenye Ofisi za TRA ili kuhuisha leseni zao kwa ajili ya mwaka 2022 na kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza mara baada ya leseni zao za sasa kufikia ukomo.

**Masharti ya Leseni;**

i). Maombi yapelekwe Ofisi ya TRA iliyo karibu kwa kutumia Fomu Na. **ITX258.01. E** inayopatikana kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) na kwenye ofisi za TRA nchi nzima. Fomu za maombi ziwasilishwe kwenye ofisi ya TRA ya mwombaji.

ii). Maombi tofauti yatafanywa kwa kila kiwanda kinachojihusisha na uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa pamoja na kila kundi la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

iii). Leseni itatolewa kwa mwombaji husika, na itatumika katika kiwanda husika na itatumika kuzalisha bidhaa iliyopewa leseni pekee.

iv). Sigara na tumbaku iliyoboreshwa vitahesabika kama kundi moja la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

v). Mzalishaji mwenye leseni hatoruhusiwa kuihamisha leseni husika, kiwanda au kutengeneza bidhaa iliyo kwenye kundi jingine (different class of excisable goods) bila kuomba na kuruhusiwa na Kamishna Mkuu.

vi). Leseni itatolewa baada ya kuwasilishwa kwa ushahidi wa malipo ya ada ya maombi ya leseni ya shilingi Laki Tano (500,000/=) kama ilivyotajwa katika Kanuni ya 4 ya Kanuni za Leseni na Usimamizi wa Wazalishaji wa Bidhaa Zinazotozwa Ushuru wa Bidhaa na/au Spiriti zenye vionjo (Denatured Spirits) za mwaka 2020

Ifahamike kuwa, kwa mujibu wa Kifungu Na. 8 na 16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, ni makosa kuzalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo bila ya kuwa na leseni halali inayotolewa na Kamishna Mkuu. Kosa hilo linaweza kupelekea adhabu ya faini au kifungo au vyote kwa pamoja. TRA itaendesha ukaguzi wa kina kubaini wazalishaji wa bidhaa husika wanaoendesha shughuli zao bila ya kuwa na leseni halali na kuwachukulia hatua stahiki.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa Na;**
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

HABARI KIMATAIFA

KIRUSI Omicron

# WHO: Shamrashamra Krismas, Mwaka Mpya ziahirishwe

**New York,** MAREKANI

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limewasihi watu kufuta baadhi ya mipango yao katika kipindi hiki cha mapumziko, kupunguza kasi ya maambukizi ya aina mpya ya virusi vya corona vya Omicron, vinavyoendelea kusambaa duniani kote.

Mkurugenzi wa WHO, Dk Tedros Ghebreyesus, amesema kufutwa kwa baadhi ya matukio yaliyopangwa ni bora, kuliko kuondoa uhai na kwamba maamuzi magumu ni lazima yachukuliwe.

**Sote tumechoka na hili janga. Wote tunataka kutumia muda wetu kuwa pamoja na marafiki pamoja na familia zetu.**

Mkurugenzi huyo, alisema kwa sasa kuna ushahidi tosha kwamba, aina ya virusi vya Omicron vinasambaa kwa kasi kushinda vya Delta, akiwataka watu kuahirisha kwa muda mipangilio yao.

"Sote tumechoka na hili janga. Wote tunataka kutumia muda wetu kuwa pamoja na marafiki pamoja na familia zetu. Sote tunataka hali irudi kawaida.

"Njia ya haraka kuweza kufanikisha hili, ni kwa sisi sote viongozi na kila mmoja kuchukua maamuzi magumu kuweza kujilinda wenyewe na kulinda wengine.

"Ni bora kufuta matukio tuliyopanga kufanya, kuliko kuyaondoa maisha...Ni bora kuacha kufanya sasa na kusherehekea baadaye kuliko kusherehekea sasa hivi na kuja kupatwa na huzuni baadaye."

Kauli hiyo ya Mkurugenzi wa WHO, imekuja wakati baadhi ya nchi ikiwamo Ufaransa na Ujerumani, zikiweka masharti makali na vikwazo vya safari katika jitihada za kujaribu kuzuia kusambaa kwa aina mpya ya virusi vya corona.

Uholanzi tayari imetangaza zuio la kutoka nje katika kipindi hiki cha msimu wa Krismas.

Ikulu ya Marekani, ilisema rais Joe Biden hana mpango wa kuweka zuio, awali mtaalamu wa magonjwa ya kuambukiza Dk Anthony Fauci, alionya safari katika kipindi cha Krismas, kwamba zitaongeza kusambaa kwa Omicron hata kwa watu ambao wamepata chanjo kamili.

Wizara ya Mambo ya Nje Marekani na Taasisi ya Kudhibiti na Kujikinga na Magonjwa (CDC), zimewashauri raia wa Marekani, kutosafiri katika nchi nane zikiwamo Hispania, Finland, Chad na Lebanon.

Uingereza nako sherehe za mwaka mpya katika baadhi ya maeneo maarufu zimefutwa, ikiwa ni hatua zilizochukuliwa kwa ajili ya usalama wa afya.

Daktari Tedros alisisitiza pia janga hilo linaweza kumalizika mwakani, iwapo asilimia 70 ya watu katika kila nchi duniani watakuwa wamechanjwa ifikapo katikati ya mwaka huo 2022.

Alisema China nchi ambayo janga hilo la mlipuko wa corona lilipoanzia mwaka 2019, ni lazima iweke wazi taarifa, ili kuweza kujulikana chanzo. **BBC**

## TPLF yadai kuondoka miji miwili

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

WAASI wa Tigray, wametangaza kuondoka katika majimbo mawili ya Amhara na Afar, Kaskazini mwa Ethiopia.

Hatua ambayo inaonekana kuwa mabadiliko makubwa katika kujaribu kumaliza mzozo unaendelea kwa miezi 13 sasa.

Msemaji wa waasi hao, Getachew Reda (pichani) kupitia ukurasa wa Twitter amesema, wamelazimika kuondoa wapiganaji wao katika majimbo hayo mawili ambayo yamekuwa kitovu cha mapambano hayo.



Marekani kupitia msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje, Ned Price alisema iwapo hatua ya waasi hao ni ya dhati na itathibitishwa, inakaribishwa katika kuelekea kupata suluhu ya kisiasa kuhusu mzozo huo, ambao umesababisha vifo vya maelfu ya watu na mamilioni kuyakimbia makazi.

Msemaji wa Serikali ya Ethiopia, Billene Seyoum, alitupilia mbali tangazo la waasi hao, kwa kile alichokieleza kuwa, ni hatua ya waasi hao kushindwa vibaya na wanajeshi wa serikali katika wiki kadhaa zilizopita.

Tangu Oktoba, mzozo wa Ethiopia ulibadilika baada ya pande zote mbili serikali na waasi, kutangaza kudhibiti miji mbalimbali na hata Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, kuamua kwenda kwenye uwanja wa vita. **RFI**



Wakazi wa Madrid wakiwa wamevalia vazi maarufu msimu wa sikukuu za Krismas la 'Santa Claus' wakifanya matembezi ya kutunisha mfuko maalumu kwa ajili ya waathiriwa wa mlipuko wa volcano Cumbre Vieja mjini Madrid, nchini Hispania, jana. **PICHA: REUTERS**

## Askari mbaroni kwa kuolewa na gwanda

**Lagos,** NIGERIA

ASKARI nchini Nigeria, amekamatwa kwa kukubali ombi la kuolewa akiwa kazini, msemaji wa jeshi amesema.

Jeshi limedai, amekiuka kanuni za maadili za kijeshi kwa kujiingiza katika mapenzi akiwa amevalia magwanda rasmi ya jeshi.

Video iliibuka wiki iliyopita ya askari huyo, akipokea pete kutoka kwa mwanamume aliyepiga magoti mbele yake, huku watazamaji wakishiriki furaha yao.

Kundi la kutetea haki za wanawake, lililishutumu jeshi kwa kumbagua.

Wanadai kwamba hatua kama hiyo haikuwa imechukuliwa dhidi ya wanajeshi wa kiume waliohusika katika maonyesho ya hadharani ya mahusiano ya kimahaba wakiwa wamevalia sare kamili za kijeshi, kikundi cha Women Empowerment and Legal Aid, kilisema.

Mwanaharakati wa haki za binadamu na aliyekuwa mgombea urais wa Nigeria, Omoyele Sowore, alilaani uamuzi wa jeshi na kuuita udhalilishaji.

Ofisa huyo, anatuhumiwa kukiuka kanuni za maadili za kijeshi kwa kujiingiza katika mapenzi, akiwa amevalia sare za jeshi. Video ilisambaa mitandaoni huku watazamaji wakishiriki furaha ya wapenzi hao.

Mwanajeshi huyo alikuwa amekubali pendekezo la ndoa kutoka kwa mwanafunzi katika mpango wa mafunzo kwa vijana wa serikali, unaojulikana kama Kikosi cha Huduma ya Vijana wa Kitaifa (NYSC).

Kama sehemu ya mpango wa lazima wa mwaka mzima kwa wahitimu kutoka vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu ya juu, hupata maagizo kutoka jeshini.

Pendekezo hilo la ndoa, lilitolewa wakati wa programu ya mafunzo katika jimbo la Kwara Magharibi.

Haijulikani tukio hilo lilifanyika lini, video yake ilisambaa wiki iliyopita.

Watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii, waliwapongeza wanandoa hao na kumsifu mwanamume huyo kwa kumchumbia. Wengine walimtania askari huyo. Msemaji wa Jeshi, Jenerali Clement Nwachukwu, aliiambia BBC kwamba mwanajeshi huyo alikiuka maadili ya jeshi, na pia sera ya mitandao ya kijamii.

"Matendo yake yalikuwa yanazuia utaratibu mzuri na nidhamu ya kijeshi. Kazi ya wakufunzi ilikuwa kuwafundisha wanachama wa kikosi cha vijana na kutojiingiza katika uhusiano wa kimahaba na yeyote kati yao," Jenerali Nwachukwu alisema.

BBCKelma Manatouma, ambaye ni mtafiti wa masuala ya siasa kutoka Chuo Kikuu cha Nanterre karibu na Paris, ameiambia AFP kwamba hiyo ni hatua muhimu kuelekea maridhiano pamoja na kukubalika kwa uhalali wa utawala wa Deby. **VOA**

# 100 WANUFAIKA AJIRA UWANJA UNAOJENGWA NA GGML GEITA

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya Watanzania 100 wamepata ajira katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo unaojengwa katika mtaa wa Magogo Halmashauri ya Mji Geita mkoani Geita kwa ufadhili wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML).

**Katika awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja huo, jumla ya Sh. bilioni 2.4 zinatumika kupitia mfuko wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR), zinazotolewa na kampuni hiyo.**

Akielezea mwenendo wa ujenzi huo hivi karibuni mjini Geita, Mhandisi Ujenzi katika mradi huo, Lt. Kanali Samuel Hagu, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ubia baina ya GGML na Halmashauri ya Mji Geita. Alitolea mfano kuwa maandalizi ya bajeti ya ujenzi ambayo ni Sh. bilioni 2.4 na usanifu wa mradi huo, vyote vimefanywa na Halmashauri ya Mji Geita kwa kushirikiana na GGML.

Alitolea mfano kuwa maandalizi ya bajeti ya ujenzi ambayo ni Sh. bilioni 2.4 na usanifu wa mradi huo, vyote vimefanywa na Halmashauri ya Mji Geita kwa kushirikiana na GGML.

"Awamu ya kwanza ya mradi wetu ilianza kutekelezwa Julai 16, mwaka huu, na matarajio yalikuwa kutekeleza kwa miezi minne, lakini bado tunaendelea kukamilisha baadhi ya vitu," alisema.

Aliongeza kuwa kwa mujibu wa taratibu zinazolenga kunufaisha jamii ya mji wa Geita, walishauriana na Kampuni ya GGML mambo mbalimbali ili kuleta tija na matunda yanayotarajiwa katika mradi huo.

"Tulikubaliana kuleta wafanyakazi karibu 50 kutoka kwenye kampuni zinazotekeleza mradi huu, lakini tukachukua nusu iliyobakia ya wafanyakazi kutoka kwenye jamii ya Mji wa Geita. Kwa hiyo tuna wafanyakazi zaidi ya 100, pia kuna huduma mbalimbali ambazo zinawanufaisha wananchi wanaozunguka mradi kama vile mama lishe.

"Kwa hiyo wanufaikaji wa moja kwa moja kupitia utekelezaji wa mradi ndio hao, lakini baadaye kutakuwa na wanufaikaji wengine kupitia uingizaji wa watu wakati uwanja utakapoanza kutumika,"alisema.

Aidha, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, amesema kampuni hiyo itaendelea kuzishirikisha kikamilifu Halmashauri ya Mji wa Geita na Halmashauri ya Geita katika miradi yote inayotekelezwa kupitia fedha za mfuko wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR).

Alisema GGML ina makubaliano ambayo waliingia pamoja na halmashauri hizo mbili ya kuwa kila mwaka watatoa Sh. bilioni 9.2 kwa ajili ya huduma za kijamii.

"Kamati ya Uwajibika wa Kampuni kwa Jamii (CSR), yenye wajumbe kutoka halmashauri hizo pamoja na Kampuni ya GGML hukaa pamoja kisha GGML wanapendekeza miradi ambayo hujadiliwa kwa pamoja na kutekelezwa kwa ushirikiano.

"Kwa hiyo hata katika ujenzi wa uwanja huu mathalani halmashauri imemtafuta mkandarasi na GGML imetoa fedha za kutekeleza mradi huo," alisema.

Halmashauri ya Mji wa Geita ilitenga eneo lenye hekta 10.4 kwa ajili ya kujenga uwanja huo wa kisasa wa michezo ambao ndani yake kutakuwa na kiwanja cha mpira wa miguu, njia za mchezo wa riadha, maeneo ya biashara na maegesho ya magari.

Uwanja huo utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuingiza watazamaji 12,000 wote wakiwa wameketi.

Katika awamu ya kwanza ya ujenzi miundombinu muhimu inayojengwa ni pamoja na jukwaa kuu, kiwanja cha mpira wa miguu, vyumba vya wachezaji, chumba cha waamuzi, chumba cha kupima wachezaji, chumba cha huduma ya kwanza, ofisi ya meneja wa uwanja na chumba cha mikutano.

Vilevile unajengwa uzio wa ukuta wa tofali na milango ya kuingilia na uchimbaji wa kisima kirefu cha maji na matangi ya kuhifadhi maji kwa ajili ya ujenzi na matumizi ya uwanja.



Ujenzi wa uwanja wa soka wa kisasa ukiendelea katika mtaa wa Magogo katika Halmashauri ya Mji wa Geita mkoani Geita kwa ufadhili wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML). **NA MPIGAPICHA WETU**

## Dodoma Jiji yaanza kuitishia nyau Yanga

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikishuka leo kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi kucheza dhidi ya Namungo FC (pichani chini), timu ya Dodoma Jiji imetamba kuchukua pointi zote sita za ugenini, ikiwamo mechi inayofuata Desemba 31, mwaka huu dhidi ya Yanga.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Moses Mpunga, amesema wamekwenda Lindi wakiwa na wachezaji wote 25 waliowasajili msimu huu, lengo likiwa ni moja tu, kuvuna pointi zote sita kwenye michezo miwili ya ugenini.

"Tuliondoka Dodoma na kikosi chote kuelekea Lindi, na tumefanya hivyo kwa sababu tunajua kuwa tuna michezo miwili migumu, wa leo dhidi ya Namungo FC, halafu baada ya hapo Desemba 31 tutacheza na Yanga. Tumedhamiria michezo yote miwili kurudi makao makuu na pointi zote sita, bila kujali ni timu gani tunacheza nayo," alisema Mpunga.

Alisema anajua ubora wa timu za Namungo na Yanga, lakini hata wao ni timu bora, kwani historia inaonyesha kuwa tangu walipopanda daraja msimu uliopita, mechi za Yanga na Dodoma Jiji hazijapata kuwa nyepesi.

Dodoma Jiji inakwenda kucheza dhidi ya Namungo ikiwa na pointi 13, kwenye nafasi ya tano, huku Namungo ikiwa nafasi ya sita kwa pointi 12 katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na Yanga yenye alama 23 kileleni.




# Kuogelea kujengewa bwawa viwango vya Olimpiki

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, amesema serikali inakusudia kujenga bwawa la kuogelea hapa nchini lenye viwango sawa na lile linalotumika katika mashindano ya Olimpiki.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Bashungwa alisema serikali imeupa mchezo huo kipaumbele na kwamba ni miongoni mwa michezo mingine inayotoa fursa kwa vijana wenye vipawa vya kuogelea kutimiza ndoto zao.

Alisema bwawa hilo la kuogelea linalotarajiwa kujengwa, litakuwa na urefu wa mita 50 sawa na mabwawa yanayotumiwa katika mashindano ya kimataifa ya Olimpiki.

"Tumejadiliana na Shirikisho la Chama cha Waogeleaji Tanzania (TSA) na kuwa na mpango mkakati mmoja kwa ajili ya mchezo wa kuogelea kuanzia hivi sasa kuelekea miaka ijayo Watanzania watarajie mageuzi makubwa katika mchezo wa kuogelea.

"Malengo yetu ni kuhakikisha vijana wanaopenda kushiriki michezo ya kuogelea, wanakwenda kwenye michezo ya kimataifa kwa viwango vya juu ili kupeperusha vema bendera yetu ya Tanzania," alisema Bashungwa.

Kuhusu kukuza vipaji vya watoto, alisema amewaasa wazazi kutotazama vipawa vya taaluma pekee yake badala yake watazame na vipaji vingine vya watoto.

"Mtoto ana vipaji kwenye michezo, hivi tuviendeleze kwa pamoja, na bahati nzuri sera ya elimu yetu ni taaluma pamoja na vipaji, kwa hali hiyo watoto wakati wapo shule tuwahimize kushiriki kwenye michezo," alisema Bashungwa.

Alisema ana wahimiza wazazi kuendeleza vipaji vya watoto wao kuanzia chini kwa sababu michezo ni ajira na inaweza kumsaidia yeye na taifa kwa baadaye.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### DZEKO, MARTIAL WAWINDWA

NEWCASTLE United wako makini kuimarisha safu yao ya ushambuliaji wakati wa dirisha dogo la Januari, huku mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial, 26 na mshambuliaji wa Inter Milan, Edin Dzeko, 35, wakiwa kwenye orodha yao. ***(Sun)***

#### KULUSEVSKI AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inaangalia uwezekano wa kuwasajili wachezaji wawili kutoka Juventus, Arthur na winga, Dejan Kulusevski, 21. ***(Marca)***

#### MYKOLENKO KUTUA EVERTON

EVERTON imekubali mkataba wa pauni milioni 17, kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa kushoto wa Dynamo Kiev na Ukraine, Vitaliy Mykolenko, 22. ***(The Mirror)***

#### KAMARA SAFI UNITED

MANCHESTER United inakaribia kumsajili kiungo wa kati mwenye thamani ya juu, Mfaransa Boubacar Kamara, mwenye umri wa miaka 22 kutoka klabu ya Marseille katika kile kitakachokuwa ni hatua ya kwanza kabisa ya Ralf Rangnick kusaini mkataba na mchezaji kama kocha wa mpito katika klabu hiyo. ***(FourFourTwo)***

#### TORRES AKARIBIA BARCA

BARCELONA imekubaliana na masharti binafsi ya Ferran Torres, 21, lakini bado haijakamilisha mkataba kwa ajili ya mshambuliaji huyo raia wa Hispania kutoka Manchester City. ***(Fabrizio Romano)***

#### RUDIGER KIMEELEWEKA MADRID

REAL Madrid wako katika mazungumzo na Antonio Rudiger, 28, yenye azma ya kusajili mlinzi huyo wa Ujerumani wakati mkataba wake utakapomalizika katika klabu ya Chelsea Juni mwakani. ***(Rudy Galetti)***

#### ARTHUR APELEKWA EVERTON

EVERTON inaweza kupewa ofa ya kiungo wa kati wa Juventus na Brazil, Arthur, 25, kama sehemu ya mkataba wowote kwa ajili ya klabu hiyo ya Italia ya kumsajili Digne. ***(Sport Mediaset - via Football Transfer Tavern)***

#### ALVAREZ ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imejiunga katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya mshambuliaji wa River Plate na Argentina, Julian Alvarez, 21. ***(Ole - via Metro)***

#### DELE AWINDWA NEWCASTLE

NEWCASTLE na West Ham wanafuatilia kwa karibu hali ya kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Dele Alli, 25. ***(Eurosport)***

#### WEST HAM YATAKA STRAIKA

KLABU ya West Ham imefanya mawasiliano na Rubin Kazan na mshambuliaji wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, 21. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND HAJAMALIZANA NA REAL MADRID - RAIOLA

**Anaweza kusubiri timu yoyote, hatuna makubaliano ya awali na yeyote, tutatafuta...**

**LONDON,** England

WAKALA wa Erling Braut Haaland, Mino Raiola, amekanusha kuwa mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund tayari amekubali kujiunga na Real Madrid msimu ujao wa joto.

**Haaland anatarajiwa kuzipambanisha klabu kadhaa kwenye vita kali ya kuwania saini yake mwishoni mwa msimu huu, dau lake likitajwa kuwa ni pauni milioni 68.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anasakwa na takriban kila klabu kubwa barani Ulaya, Real Madrid ikiwa ni miongoni ikiungana na Barcelona, Manchester United, Manchester City, Chelsea, Bayern Munich, Juventus, Paris Saint-Germain, na Liverpool.

Mkurugenzi Mtendaji wa Dortmund, Hans-Joachim Watzke, alithibitisha wiki hii kwamba Real Madrid wanavutiwa na Haaland, na baadhi ya ripoti zilidai kuwa makubaliano tayari yanaweza kutekelezwa.

Lakini wakala wake, Raiola amekanusha tetesi hizo na kusisitiza kuwa mteja wake atachagua klabu ambayo ni bora kwake, na pia anaweza kubaki Dortmund.

"Haaland anaweza kusubiri timu yoyote. Hatuna makubaliano ya awali na klabu yoyote. Tutatafuta chaguo bora zaidi, na pia sijakataa mwaka mwingine ndani ya Borussia Dortmund," alisema Raiola akinukuliwa na Daily Mail.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amefunga mabao 19 na asisti tano katika mechi 16 msimu huu, na ana mabao 76 katika michezo 75 aliyoichezea Dortmund kwa jumla.

MECHI KALI
HOME
AWAY
LORIENT
6.52 | 4.65 | 1.44
PARIS ST GERMAIN
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 804

# TUCHEL AMTAKA NEVES CHELSEA



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ameripotiwa kumwania kiungo wa Wolves, Ruben Neves wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari.

Tuchel anataka kuboresha safu yake ya kiungo baada ya N'Golo Kante na Mateo Kovacic kukosa sehemu kubwa za michezo ya Ligi Kuu msimu huu, huku Saul Niguez akiwa bado hajaanza kuonyesha makali yake.

Taarifa zinaeleza kuwa Neves, amewekwa kwenye orodha ya wachezaji ambao wanapigiwa chapuo na kocha huyo kutoka nchini Ujerumani.

Kwa mujibu wa ripoti ya Todofichajes, Tuchel anamwona Neves ni mtu sahihi wa kuwamo kwenye kikosi chake.

Hata hivyo, Wolves hawapo tayari kumwachia nyota huyo katikati ya msimu na wanaweza kukaa kujadili hilo kama itawekwa mezani ofa inayofikia pauni milioni 40.

# *Ligi Kuu EPL ratiba kuendelea kawaida*

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England (EPL), itaendelea na ratiba yake kama kawaida licha ya mlipuko mpya wa virusi vya corona na kusababisha michezo kadhaa kuahirishwa.

Klabu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo zilikutana Jumatatu na kupitisha azimio moja la kuendelea na ligi kama kawaida.

Ilitarajiwa huenda michezo itakayochezwa baada ya Sikukuu ya Krismas ingeahirishwa, lakini hakuna kura iliyopigwa ya kukubali kuhairisha michezo hiyo.

Michezo ya wiki ya 20 itakayoanza Desemba ilitarajiwa kuwa ingeahirishwa ili kupunguza presha, lakini klabu zimekubaliana kama wachezaji 13 wako sawa akiwamo kipa mchezo uchezwe.

Pia kuna mazunguzo kati ya klabu na mamlaka kuiondoa michezo ya Kombe la FA ya mzunguko wa tatu na nne na kuipunguza michezo ya nusu fainali ya EFL (Carabao Cup) kuchezwa mchezo mmoja tu na si miwili kama ilivyo kawaida.

Michezo mitano kati ya sita ya Jumamosi iliahirishwa, Chelsea waliomba nao mchezo wao wa Jumapili dhidi ya Wolves uahirishwe na mamlaka ilikataa, pia Liverpool walikuwa miongoni mwa timu zilizotaka michezo ya wiki 20 kuahirishwa.

## HABARI MICHEZO


# 4,667,160

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/2021 | 18:00 | Peterborough vs Reading | 2.37 | 3.28 | 2.84 |
| 02. 26/12/2021 | 18:00 | Millwall vs Swansea | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 03. 26/12/2021 | 18:00 | Hull City vs Blackburn | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 04. 26/12/2021 | 18:00 | Preston vs Sheffield Utd | 2.90 | 3.25 | 2.34 |
| 05. 26/12/2021 | 18:00 | Portsmouth vs Oxford Utd | 2.43 | 3.28 | 2.75 |
| 06. 26/12/2021 | 18:00 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 07. 26/12/2021 | 18:00 | Cheltenham vs Plymouth | 2.99 | 3.33 | 2.24 |
| 08. 26/12/2021 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Charlton | 2.70 | 3.24 | 2.50 |
| 09. 26/12/2021 | 18:00 | Dundee Utd vs Hibernian | 2.90 | 3.15 | 2.42 |
| 10. 26/12/2021 | 18:00 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.75 | 3.55 | 2.43 |
| 11. 26/12/2021 | 18:00 | Burnley vs Everton | 2.48 | 3.15 | 2.95 |
| 12. 26/12/2021 | 18:00 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 13. 26/12/2021 | 18:00 | Hamilton vs Kilmarnock | 2.72 | 3.26 | 2.43 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 22 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 3450 | Tuzlaspor vs Erzurum BB | 2.71 | 3.29 | 2.35 |
| 15:30 | 4815 | Singapore vs Indonesia | 3.27 | 3.22 | 2.07 |
| 16:30 | 4388 | TS Galaxy FC vs Stellenbosch | 2.60 | 2.90 | 2.85 |
| 17:00 | 2131 | Hatayspor vs Konyaspor | 2.36 | 3.25 | 2.91 |
| 17:00 | 3030 | Leca FC vs USC Paredes | 1.92 | 3.28 | 3.66 |
| 17:00 | 3800 | Sivasspor vs Caykur Rizespor | 1.58 | 3.91 | 5.34 |
| 18:00 | 2790 | Baroka FC vs Bloemfontein Celtic | 3.09 | 2.99 | 2.37 |
| 18:00 | 3065 | Chippa Utd vs Sekhukhune United | 2.60 | 2.85 | 2.90 |
| 18:00 | 4402 | Moroka Swallows FC vs Golden Arrows | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 18:30 | 1435 | SuperSport Utd vs Cape Town City | 2.05 | 2.99 | 3.88 |
| 18:30 | 4722 | Sassuolo vs Bologna | 2.03 | 3.70 | 3.35 |
| 18:30 | 4981 | Venezia vs Lazio | 4.10 | 3.80 | 1.81 |
| 20:00 | 4531 | Fatih Karagumruk vs Fenerbahce | 3.20 | 3.40 | 2.14 |
| 20:00 | 5103 | Gaziantep BB vs Alanyaspor | 2.34 | 3.35 | 2.86 |
| 20:00 | 5219 | Olympiakos vs Levadiakos | 1.06 | 8.49 | 25.08 |
| 20:30 | 1123 | Inter vs Torino | 1.32 | 5.37 | 8.55 |
| 20:30 | 1938 | Kaizer Chiefs vs Maritzburg Utd | 1.50 | 4.02 | 6.08 |
| 20:30 | 4107 | Roma vs Sampdoria | 1.57 | 4.31 | 5.21 |
| 20:30 | 5714 | Verona vs Fiorentina | 2.81 | 3.46 | 2.41 |
| 20:45 | 2247 | Willem II Tilburg vs NEC Nijmegen | 2.43 | 3.23 | 2.79 |
| 20:45 | 5599 | Heerenveen vs Feyenoord | 5.49 | 4.32 | 1.50 |
| 21:00 | 4800 | Granada vs Atletico Madrid | 5.78 | 3.79 | 1.60 |
| 22:00 | 1497 | Heracles Almelo vs Cambuur | 2.02 | 3.63 | 3.23 |
| 22:00 | 3471 | Mechelen vs Eupen | 1.78 | 3.86 | 3.81 |
| 22:30 | 2127 | KAA Gent vs Standard Liege | 1.53 | 4.10 | 5.28 |
| 22:45 | 1050 | Brentford vs Chelsea | 4.74 | 3.55 | 1.72 |
| 22:45 | 1210 | Hibernian vs Aberdeen | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 22:45 | 1834 | Tottenham vs West Ham | 2.30 | 3.25 | 3.01 |
| 22:45 | 2041 | Napoli vs Spezia | 1.26 | 6.00 | 10.00 |
| 22:45 | 2648 | St Johnstone vs Ross County | 2.47 | 3.01 | 2.96 |
| 22:45 | 2712 | Crusaders Belfast vs Glenavon | 1.49 | 4.25 | 5.21 |
| 22:45 | 2716 | Montrose vs Peterhead | 1.84 | 3.67 | 3.72 |
| 22:45 | 2997 | Empoli vs AC Milan | 4.11 | 4.01 | 1.76 |
| 22:45 | 3972 | Liverpool vs Leicester | 1.65 | 3.95 | 4.64 |
| 22:45 | 5109 | St Mirren vs Celtic | 11.88 | 6.14 | 1.21 |
| 22:45 | 5335 | Coleraine FC vs Glentoran Belfast | 2.38 | 3.47 | 2.55 |
| 23:00 | 1058 | Nice vs Lens | 2.10 | 3.44 | 3.34 |
| 23:00 | 1799 | St Etienne vs Nantes | 2.54 | 3.19 | 2.79 |
| 23:00 | 2313 | Montpellier vs Angers | 2.19 | 3.29 | 3.29 |
| 23:00 | 2317 | Lyon vs Metz | 1.35 | 5.38 | 7.37 |
| 23:00 | 2364 | Bordeaux vs Lille | 3.94 | 3.69 | 1.85 |
| 23:00 | 2553 | Monaco vs Rennes | 2.22 | 3.38 | 3.14 |
| 23:00 | 3171 | Clermont Foot vs Strasbourg | 2.84 | 3.34 | 2.41 |
| 23:00 | 4633 | Ajax vs Fortuna Sittard | 1.02 | 13.71 | 39.19 |
| 23:00 | 4774 | Troyes vs Brest | 2.47 | 3.24 | 2.84 |
| 23:00 | 4952 | Marseille vs Reims | 1.66 | 3.69 | 5.18 |
| 23:00 | 4958 | Lorient vs Paris St Germain | 6.52 | 4.65 | 1.44 |
| 23:00 | 5662 | Utrecht vs Twente | 1.73 | 3.77 | 4.21 |
| 23:30 | 2033 | Athletic Bilbao vs Real Madrid | 3.15 | 3.35 | 2.25 |
| 23:45 | 1376 | Casa Pia Atletico vs Sporting Lisbon | 9.41 | 5.19 | 1.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.





# SAIDO: UBINGWA YANGA SC UNAWEZEKANA MSIMU HUU

**Na Dennis Fussi**

KIUNGO wa Yanga, Saido Ntibazonkiza, amesema bado kikosi chao kina nafasi kubwa ya kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu 2021/22.

Baada ya kuifunga Tanzania Prisons Jumapili, Yanga imeendelea kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa kufikisha alama 23, ikifuatiwa na Simba yenye pointi 18.

**Saido ambaye alisajiliwa Yanga wakati wa dirisha dogo msimu wa 2020/21, amesema wanaendelea kupambana ili kufanikisha azma ya kutwaa ubingwa na kasi waliyonayo sasa inawaaminisha hakuna cha kuwazuia.**

"Bado mapambano yanaendelea na tutapambana kwa jasho kupata ushindi ili kufikia lengo la kutwaa ubingwa," alisema.

"Mashabiki wanapenda kuona sisi tunashinda mechi zetu hili hata sisi tunalipenda pia, kwani ili kupata pointi tatu ni lazima kushinda pale ambapo tunacheza, tunaamini kwamba tutafanya vizuri."

Katika mabao 14 ambayo yamefungwa na Yanga kwenye michezo ya Ligi Kuu, Saido ametupia mabao mawili na ana pasi moja ya bao.



Kundi la Tanzania Philharmonic Society (TPS), likitoa burudani kwenye uzinduzi wa Tamasha la Christmas Carols jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Kwaya zanogesha Christmas Carols*

**Na Sabato Kasika**

KWAYA mbalimbali na waimbaji nyota wa muziki wa injili, akiwamo Rose Mhando, wamepamba uzinduzi wa tamasha lililopewa jina la 'Christmas Carols 2021' ulilofanyika Mlimani City jijini Dar es Salaam juzi.

Baadhi ya waimbaji wengine walikuwa ni pamoja na Goodluck Gozbert, Beda Andrew, Ambwene Mwasongwe, Barnaba Classic na kwaya kama KKKT Kijitonyama, Bwagamoyo to Jesus, Ufunuo na Baragumu.

Vilevile katika uzinduzi wa tamasha hilo, walikuwapo waimbaji wa Kundi la Tanzania Philharmonic Society (TPS) na kwaya nyingine nyingi zilizoalikwa kutoa burudani kuanzia mchana hadi usiku.

Meneja Masoko wa Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo, amesema tamasha la mwaka huu linatarajiwa kuwa tofauti kwa kulifanya kwa ajili ya kumshukuru Mungu kwa kuwavusha katika mambo mengi.

"Tumeshirikiana na wenzetu katika tamasha hili, sisi tunatangaza mti wetu wa Krismasi uliotengenezwa kwa maboksi, watu wanaweza kuja kusimama mbele yake na kupiga picha mbalimbali za ukumbusho," alisema Kabula.

Alisema tamasha hilo litaendelea kipindi chote cha sikukuu za mwisho wa mwaka katika mikoa mbalimbali nchini, ikiwamo ya Morogoro, Dodoma, Mwanza na kule Bonite Kilimanjaro ili Watanzania wapate vitu vyao.

"Clouds wana Christmas Carols na sisi tuna Christmas Caravan, ni ukweli ni kwamba Christmas haiwezi kukamilika bila Coca-Cola, hivyo ninaamini kwamba wadau wataburudika vya kutosha," alisema.

# Michezo

Jumatano Novemba 22, 2021

Nipashe




## Haaland hajamalizana na Real - Raiola

UKURASA 21

WAJE TU...



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini. Jumapili wiki hii timu hiyo itaikaribisha Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTBA**

## Simba yafunguka afya za wachezaji

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI afya za wachezaji wa Simba ikielezwa kuendelea vema kutokana na kukabiliwa na changamoto za homa, mafua na kikohozi, wachezaji 15, benchi la ufundi, madaktari na wafanyakazi wa Mtibwa Sugar nao wamekumbwa na ugonjwa huo.

Klabu ya Azam nayo imeripoti baadhi ya wachezaji wake kupatwa na tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, amesema kuwa wachezaji wa timu hiyo wanaendelea vizuri, lakini bado wapo kwenye uangalizi wa madaktari pamoja na wataalamu wa afya hadi hapo watakaporejea kwenye hali yao ya kawaida.

"Wachezaji wetu wanaendelea vizuri kwa sasa, lakini bado wapo kwenye uangalizi wa madaktari wa wataalamu wa afya hadi pale watakaporudi kwenye hali zao za kawaida," alisema.

Aidha, alisema wachezaji wao wanaendelea na mazoezi kwa sababu haiwezekani wakakaa bila kucheza, labda benchi la ufundi tu ambalo nalo pia lilikumbwa na changamoto hiyo.

"Huu ni ugonjwa, nashangaa watu wanaongea vitu wasivyovielewa, kwa hali yoyote haiwezekani Simba ambayo inatoka Dar es Salaam, Tanzania kwenda kucheza na Misri, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na timu kubwa kama Al Ahly na zingine, wakati mwingine inashinda nje ya nchi, leo hii iogope kwenda kucheza na Kagera Sugar au Tabora na KMC?" Alihoji Mangungu.

# YANGA RASMI YAMNASA NKANE, SURE BOY AITWA

### ●●● Ripoti ya Nabi yalenga nyota watatu wazawa na Muivory Coast mmoja, asema lazima...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI kiungo wa Azam FC, Salum Aboubakar 'Sure Boy' akiitwa mezani kuwasilisha barua rasmi ya kuvunja mkataba baada ya kutoa taarifa kwa mdomo, Klabu ya Yanga tayari 'imepiga bao' kwa kumnasa winga wa Biashara United, Dennis Nkane katika usajili huu wa dirisha dogo, imeelezwa.

**Akizungumza na gazeti hili jana moja kwa moja kutoka Musoma mkoani Mara, Meneja wa Klabu ya Biashara United, Frank Wabare, alithibitisha kuondoka kwa mchezaji huyo na kudai mazungumzo kati yao na Yanga yamefikia asilimia 99.**

"Mazungumzo kati yetu na Yanga yanaendelea vizuri, nina imani kila kitu kitakuwa sawa, japo mpaka sasa Dennis bado tupo naye mipango ikikamilika tutamruhusu kwenda kuendelea na maisha mengine," alisema Wabare.

Hata hivyo, alisema baada ya kuondoka mchezaji huyo nafasi yake itajazwa na wachezaji wengine ambao wanaendelea kufanya nao mazungumzo ili ikiwezekana waweze kuwasajili katika usajili huu wa dirisha dogo unaotarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani.

Kwa upande wa Sure Boy, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', amesema kati ya wachezaji watatu waliosimamishwa kutokana na utovu wa nidhamu, wawili ambao ni Mudathir Yahaya na Aggrey Morris, wamerejea kwenye kikosi, lakini Sure Boy yeye ameuambia uongozi kwa mdomo kuwa hawezi kuendelea tena kuichezea timu hiyo na anataka kuondoka.

"Ametuambia kwa mdomo, kwa hiyo tumemwambia aandike barua rasmi ya kuomba kuondoka ili tukae na wanasheria wetu tuangalie ni vitu gani vinatakiwa vifanyike kabla ya hayo anayotaka ili aweze kwenda anapohitaji," alisema Zaka Zakazi.

Habari zinaeleza kuwa mchezaji huyo anatakiwa na klabu ya Yanga, na itakuwa si mara ya kwanza kutakiwa kwani hata mwanzoni mwa msimu huu ilikuwa hivyo, lakini ilishindikana baada ya Yanga kushindwa kuvunja mkataba wake.

Katika hatua nyingine, ripoti ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, imeelezwa kwamba amependekeza katika dirisha hili dogo kuongezwa wachezaji wanne na hadi sasa mchezaji ambaye kwa uhakika klabu hiyo imemnasa ni Nkane.

Nafasi ambazo Nabi amependekeza kuboreshwa ni kuongezwa mshambuliaji mmoja, beki wa kati mmoja, kipa na winga husussan anayetumia mguu wa kushoto ili kuziba nafasi ya Yacouba Songne ambaye ni majeruhi.

"Nimependekeza nafasi ninazohitaji ikiwamo winga mzawa pamoja na nafasi ya kipa, kuna wakati lazima klabu kubwa kama Yanga ifikirie kuwaongezea thamani wachezaji wazawa," alisema Nabi.

Hata hivyo, taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jana kutoka ndani ya uongozi wa Yanga, zilieleza kuwa tayari wameanza kufanyia kazi mapendekezo ya Nabi na muda si mrefu watawatangaza nyota waliowasajili.

"Tayari tumeshamalizana na wachezaji wawili wazawa, ni mapema sana kutaja majina yao na yupo nyota wa kigeni anayetoka nchini Ivory Coast," kilieleza chanzo chetu.

Wakati huo huo kikosi cha Yanga kimeingia kambini kwa ajili ya kujiwinda na mechi dhidi ya Biashara United itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

***Imeandaliwa na Shufaa Lyimo, Adam Fungamwango na Saada Akida***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >